YALIYOMO

MADA	UKURASA
SEHEMU YA KWANZA	4
1.0 UTANGULIZI	4
1.1 MUUNDO WA KAMATI	4
1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI	5
SEHEMU YA PILI	6
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO	6
2.1 IDARA ZA WAZARA YA FEDHA NA MIPANGO	6
2.2 TUME YA MIPANGO	6
2.3 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA	6
2.4 TAASISI ZA MUUNGANO	7
2.5 UKUSANYAJI MAPATO JULAI HADI DISEMBA	7
2.6 MAMLAKA YA UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI (ZIPA)	8
2.7 JUMBA LA TRENI	9
2.8 TUME YA MIPANGO	9
2.9 BENKI KUU YA TANZANIA (BOT) - TAWI LA ZANZIBAR	10
2.9.1 GAWIO LINALOTOKANA NA MAPATO YA BENKI KUU	11
2.10 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)	12
2.10. 1 TAWI LA CHAKECHAKE NA MKOANI	12
2.11 BENKI YA CRDB	13
2.12 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA	13
2.13 SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR - TAWI LA PEMBA	14
2.14 SHIRIKA LA BIMA - TAWI LA MWANZA	15
SEHEMU YA TATU	16
WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO	16

3.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI 16
3.2 SHIRIKA LA TAIFA LA BIASHARA (ZSTC) 18
3.2.1 FIDIA YA WAHANGA WA KARAFUU 18
3.2.2 ZIARA YA KAMATI - DUBAI 18
3.2.3 TAWI LA BIASHARA ZA KIMATAIFA NCHINI DUBAI 20
3.2.4 TAWI LA ZSTC - DAR ES SALAAM 21
3.2.5 SHAMBA LA ZSTC - MTAKATA 22
3.3 UKAGUZI WA VIPIMO NA MIZANI 23
3.4 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI 24
3.5 KIWANDA CHA USHONI CHA IDARA MAALUM ZA SMZ 25
3.6 MAMLAKA YA KUSIMAMIA UZALISHAJI KWA AJILI YA USAFIRISHAJI (EPZA) UBUNGO DAR - ES - SALAAM 26
SEHEMU YA NNE 27
WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI 27
4.1 MUUNDO WA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI 27
4.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 27
4.3 UKODISHAJI WA MASHAMBA YA SERIKALI YA MIKARAFUU PEMBA KWA MSIMU WA MWAKA 2017 28
4.3.1 MALENGO YA UKODISHAJI NA UKUSANYAJI MAPATO 28
4.3.2 TAASISI ZILIZOSHIRIKI KATIKA UKODISHAJI 29
4.3.3 GHARAMA ZA UKODISHAJI 29
4.3.5 MATOKEO YA UKODISHAJI NA UKUSANYAJI MAPATO 30
4.4 MALIPO YA FEDHA INAYOTOKANA NA HUDUMA YA SHAMBA (VIFUTAJASHO) 32
4.5 MSITU WA HIFADHI YA TAIFA WA KIWENGWA 33
4.6 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI 34
4.7 MAENDELEO YA UVUVI 35

4.7.1 UZALISHAJI WA ZAO LA MWANI 35
4.7.2 SHUGHULI ZA UANIKAJI DAGAA 36
4.8 MAENDELEO YA KILIMO 37
4.8.1 UENDELEZWAJI WA SHAMBA LA RAZABA 37
4.8.2 KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO - MATANGATUANI 38
4.9 KILIMO CHA MPUNGA WA UMWAGILIAJI MAJI 38
4.9.1 BONDE LA CHEJU 39
4.9.2 BONDE LA MANGWENA 39
4.9.3 BONDE LA MPUNGA LA UKELE 40
4.10 SHAMBA LA MIKARAFUU MAKUWE 41
4.11 WAKALA WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO 42
4.12 UATIKAJI WA MICHE 43
4.12.1 KITALU CHA MWERA 43
4.12.2 KITALU CHA CHANJAANI MWANATOJO 44
4.13 WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI - PEMBA. 44
SEHEMU YA TANO 46
5.1 HITIMISHO 46

RIPOTI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LAWAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu Kanuni ya 106, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016, na majukumu yake yameelezwa kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika;
iv. Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
v. Kuchambuwa mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambuwa ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika;

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ina jukumu la kusimamia Wizara zifuatazo:

- Wizara ya Fedha na Mipango;
- Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; na
- Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ina Wajumbe saba na Makatibu wawili, naomba sasa niwataje kwa majina Wajumbe na Makatibu hao kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe

6. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe
7. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
8. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu
9. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Katika utekelezaji wa Kanuni ya 108, Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, hadi Kamati inawasilisha ripoti yake mbele ya Baraza hili tukufu ilifanya kazi zake kwa mizunguko mitatu kwa muda wa wiki sita, kati ya Unguja na Pemba.

1. Mzunguko wa kwanza kuanziaTarehe 03/04/2017 hadi 06/04/2017 Unguja na Tarehe 10/04/2017 hadi tarehe 14/04/2017 Pemba.
2. Mzunguko wa pili kuanzia Tarehe 14/08/2017 hadi tarehe 24/08/2017 Unguja.
3. Mzunguko wa tatu kuanzia Tarehe 13/11/2017 hadi tarehe 17/11/2017 Unguja na Tarehe 20/11/2017 hadi 24/11/2017 Tarehe Pemba.

Ripoti hii imeandaliwa kwa kutumia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Kanuni ya Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2016), Taarifa za utekelezaji za Wizara, Taarifa za utekelezaji wa maagizo ya Kamati na Ripoti mbalimbali zilizotokana na tafiti zilizofanywa na Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

SEHEMU YA PILI

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Wizara ya Fedha na Mipango imeundwa na Idara kumi (10), Tume ya Mipango yenye Idara nne (04), Taasisi Tisa (09) zinazojitegemea na Taasisi nne (04) za Muungano zinazofanya kazi hapa Zanzibar. Idara na Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:

2.1 IDARA ZA WAZARA YA FEDHA NA MIPANGO

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
ii. Idara ya Utawala na Uendeshaji;
iii. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali;
iv. Idara ya Bajeti;
v. Idara ya Fedha za Nje;
vi. Idara ya Mitaji ya Umma;
vii. Idara ya Hesabu za Ndani;
viii. Idara ya Fedha za Kodi;
ix. Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma; na
x. Ofisi Kuu Pemba.

2.2 TUME YA MIPANGO

i. Idara ya Uratibu wa Mipango ya Kitaifa, maendeleo ya kisekta na kupunguza umasikini;
ii. Idara ya Maendeleo ya Watendakazi;
iii. Idara ya Ukuzaji Uchumi; na
iv. Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini.

2.3 TAASISI ZINAZOJITEGEMEA

i. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB);
ii. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ);
iii. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi (ZIPA);
iv. Mfuko wa Barabara (ZFR);
v. Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC);
vi. Bodi ya Rufaa za Kodi (Tax Appeal Board);
vii. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF);
viii. Mahkama ya Rufaa za Kodi; na
ix. Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

2.4 TAASISI ZA MUUNGANO

i. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA);
ii. Mamlaka ya Bima Tanzania (TIRA);
iii. Benki Kuu ya Tanzania (BOT); na
iv. Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC) - Tawi la Zanzibar.

2.5 UKUSANYAJI MAPATO JULAI HADI DISEMBA

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya Tzs. 1,059.4 bilioni zikiwemo Tzs. 649.4 bilioni zinazotokana na vyanzo vya ndani na 380 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Tzs. 30 bilioni ni mikopo ya ndani. Hadi kufikia Disemba 2017, jumla ya Tzs. 459.47 bilioni zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 63 ya makadirio ya Tzs. 732.87 bilioni ya kipindi hicho na asilimia 42 ya makadirio ya mwaka. Maelezo ya kina kuhusu makusanyo ya Serikali kwa kipindi cha Julai hadi Disemba yanaonekana katika Jadueli lifuatalo:

Jadueli Namba. 1: Mapato kwa kipindi cha Julai - Disemba 2017/2018

TARAKIMU NI (TZS)

	Bajeti	Makadirio	Halisi	UTEKELEZAJI	
				% ya Makadirio	% ya Bajeti
Mapato ya kodi:	627,014.00	311,844.26	298,624.71	96%	48%
Bodi ya Mapato (ZRB)	347,290.00	174,690.17	161,849.88	93%	47%
Mamlaka ya Mapato (TRA)	258,724.00	126,654.09	126,274.83	100%	49%
Mapato ya PAYE - SMT	21,000.00	10,500.00	10,500.00	100%	50%
Mapato Mengineyo:	**78,800.00**	**41,027.28**	**41,678.40**	**102%**	**53%**
Gawio la BOT	3,000.00				
Gawio Mashirika	3,000.000				
Mapato ya Mawizara	42,800.00	21,027.28	21,678.19	103%	51%
Mapato ya Ndani	30,000.00	21,000.00	21,000.21	100%	67%
Mapato kutoka nje:	**380,000.00**	**380,000.00**	**119,167.03**	**31%**	**31%**
Misaada (Misaada)	82,000.00	41,000.00	21,000.00	51%	26%
Mikopo ya Nje (Grant)	298,000.00	149,000.00	95,700.00	64%	32%
MDRI			1,671.05		
GBS	100T		796.0		
JUMLA KUU	**1,085,814.00**	**732,871.54**	**459,470.14**	**63%**	**42%**

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Kwa upande wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha miezi sita yamefikia jumla ya Tzs. 463.66 bilioni yakijumuisha matumizi ya kazi za kawaida ni Tzs. 590.70 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya kipindi hicho na asilimia 51 ya makadirio ya mwaka. Aidha, matumizi ya kazi za maendeleo ni jumla ya Tzs. 165.34 bilioni sawa na asilimia 68 ya ukomo na asilimia 33 ya makadirio ya mwaka.

2.6 MAMLAKA YA UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI (ZIPA)

Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi ni Mamlaka ambayo imeundwa chini ya Sheria Namba 11 ya mwaka 2004. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa makusudi iliamua kuunda chombo hiki kwa kutambua umuhimu wa sekta binafsi ama kutoka ndani ya Zanzibar au nje kujitokeza kuwekeza na kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu. Kuwepo kwa Mamlaka hiyo, kumesaidia wawekezaji wengi kuamua kuja Zanzibar kuwekeza katika masuala ya uendeshaji wa hoteli, ujenzi wa maeneo ya kufurahishia watoto na ujenzi wa nyumba za kisasa za makaazi

CHANGAMOTO

1. Tatizo sugu linalokwamisha jitihada za uwekezaji Zanzibar ni kuwa na watendaji wakuu wenye kauli tofauti katika Taasisi za Serikali. Hali hii inapelekea urasimu katika taratibu za uwekezaji nchini na hivyo kuwafanya wawekezaji kuchukua muda mrefu wa kufuatilia vibali na mara kadhaa huishia njiani bila ya mafanikio.
2. Ingawa Serikali imeanzisha kitengo cha ushughulikiaji wa vibali vya ujenzi 'Development Control Unit' kwa ajili ya usimamizi wa vibali vya ujenzi nchini, bado maombi ya wawekezaji yanachukua muda mrefu.
3. Uchakavu wa majengo ya maeneo huru ya Amani (Aman Industrial Park) unapelekea kutumika fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo siku hadi siku.
4. Ucheleweshwaji wa utoaji wa vibali kwa wawekezaji unazorotesha na kuwavunja moyo wawekezaji.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) kuharakisha mpango wake wa kuanzisha kituo cha kuhudumia wawekezaji (one stop center) ambacho kitawarahisishia kazi na kuwaepusha wawekezaji na mizunguuko isiyo ya lazima.
2. Kamati inaishauri Serikali kukiweka Kitengo cha Usimamizi wa Vibali vya Ujenzi (DCU) chini ya usimamizi wa ZIPA ili kuifanya kazi ya utoaji wa vibali kuwa rahisi na yenye ufanisi wa hali ya juu.
3. Kamati inashauri Wizara kupitia ZIPA ihakikishe inayafanyia matengenezo ya mara kwa mara majengo ya maeneo huru ya Amani (Aman Industrial Park) na kutafuta muwekezaji haraka iwezekanavyo ili kujenga majengo ya kisasa ya uwekezaji.
4. ZIPA ihakikishe inakamilisha 'Master Plan' ya Micheweni ili wawekezaji waweze kuitumia.
5. ZIPA ihakikishe miradi miwili iliyopo Pemba inatekelezwa.
6. Mamlaka iharakishe inaliendeleza eneo la Michenzani lililokaa bila shughuli yoyote ya kiuchumi kufanyika.

2.7 JUMBA LA TRENI

Serikali iliamua kulifanyia matengenezo makubwa jumba la treni (Chawl Building), baada ya kuonekana kuwa jengo lipo katika hali mbaya na wakati wowote linaweza kuleta madhara kwa wafanyabiashara. Matengenezo hayo yanakusudiwa kufanywa ili kuliongezea ubora na haiba ya jengo bila ya kubadilisha matumizi. Baada ya kukamilika kwake, jengo linatarajiwa kuwa na maduka 52, sehemu 2 za ATM, sehemu ya kuswalia wanawake, nyumba 10 za kuishi (2 za vyumba viwili na 8 za chumba kimoja) sehemu za Ofisi, Supermarket, sehemu ya kufanyia mazoezi (Gymnasium) na Mkahawa (Restaurant). Mradi pia umezingatia uwepo wa watu wenye mahitaji maalum, hivyo umeweka "ramp" itayowawezesha kufika katika ghorofa ya chini na kuweka "lifti" ambayo itasaidia kuwafikisha katika ghorofa zilizobakia.

Kazi ya matengenezo ya jumba hilo ilianza rasmi tarehe 2 Novemba 2016, baada ya Mkandarasi kukabidhiwa jengo. Mradi huo unatarajiwa kukamilika ndani kipindi cha miezi kumi na nane (18) kuanzia Novemba 2016 hadi Mei 2018. Gharama za mradi hadi kukamilika kwake zinatarajiwa kuwa ni Tzs. 11.2 bilioni. Hadi Kamati ilipotembelea mradi huo malipo ya jumla ya Tzs. 4 bilioni sawa na asilimia 36 ya gharama zote zimelipwa.

CHANGAMOTO

1. Kuongezeka kwa gharama za mradi kwa kufuatana na sheria za ujenzi za Mji Mkongwe hali inayopelekea kuongezeka kwa muda wa kurejesha fedha zilizotumika (Pay Back Period).
2. Uhaba wa maeneo ya maegesho ya magari kwa watumiaji na wafanyabiashara watakaohitaji kupatiwa huduma katika jumba hilo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaushauri Mfuko kusimamia vyema ujenzi wa jumba la Treni ili ukukidhi mahitaji ya kuwa na jengo la kisasa ambalo halikiuki vigezo vya Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkonge na UNESCO.
2. Kamati inauagiza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) uhakikishe unakamilisha Mradi huo kwa wakati uliopangwa.
3. Baada ya kukamilika Mradi huo, Kamati inautaka Mfuko kuwapa kipaumbele waliokuwa wakimiliki nyumba na maduka yaliyomo ndani ya jumba hilo.

2.8 TUME YA MIPANGO

Tume ni chombo kinachojitegemea kilichoundwa na kifungu cha 125 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Tume ya Mipango Namba 3 ya mwaka 2012 ambacho kimekabidhiwa jukumu kuu la kutayarisha, kuratibu na kutekeleza mipango ya kiuchumi na kijamii Zanzibar kwa lengo la kuleta maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Tume imekadiriwa kutumia jumla ya Tzs. 9,430,837,000 bilioni. Kati ya fedha hizo, Tzs. 4,699,600 milioni ni kwa ajili ya kazi za

Kawaida na jumla ya Tzs. 4,731,237 milioni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Disemba 2017, Tume iliomba kupatiwa jumla ya Tzs. 58,326,017.00 bilioni na kupatiwa jumla ya Tzs. 55,721,700.00 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 96 ya maombi hayo.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Tume inasimamia jumla ya miradi minane (8) ambayo inaendelea kutekelezwa kwa kila robo mwaka. Kadhalika, hadi kufikia Disemba, 2017 jumla ya Miradi 42 inaendelea kutekeleezwa na Sekta mbali mbali nchini.

CHANGAMOTO

1. Bado mfumo wa uongozi kwa njia ya ugatuzi haujafahamika kwa baadhi ya Viongozi na wananchi kwa ujumla. Hali hii itapelekea ugumu wa uendeshaji wa mfumo huo kwani unahitaji fikra ya pamoja baina ya Taasisi moja na nyengine.
2. Upungufu mkubwa wa fedha kwa ajili ya uendeshaji na utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Tume yakiwemo ya kuwapatia uelewa wananchi kuhusu MKUZA III kwa nchi nzima.
3. Kukosekana kwa jengo rasmi la Tume ya Mipango ambapo hadi sasa Tume inatumia majengo ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi.
4. Kuwepo kwa mashirikiano yasiyoridhisha baina ya Tume ya Mipango Zanzibar na Tume ya Mipango ya Tanzania Bara hususan katika uwasilishaji wa mapendekezo ya maandiko ya Miradi ya Maendeleo kwa Wahisani. Hali hii inarudisha nyuma dhana nzima ya kuwepo uaminifu katika utendeaji wa Tume hizi mbili.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Tume ya Mipango iendelee na utoaji wa elimu kwa wadau wa sekta mbalimbali ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kufuata Sera ya Ugatuzi wa Madaraka Mikoani.
2. Kamati inaishauri Tume ya Mipango Zanzibar kuwa na ushirikiano wa karibu na Tume ya Mipango ya Tanzania Bara ili kuzifanya pande mbili hizi kupashana habari na kupeana miongozo itakayopelekea kuwasilisha kwa washirika wa maendeleo miradi ambayo inaendana na masharti yanayokubalika kwa maslahi ya Mataifa yetu.
3. Kwa vile Karafuu inachangia sehemu kubwa katika pato letu la Taifa, Kamati inaitaka Tume ya Mipango kufanya utafiti wa kina ili kujua ni kwa kiwango gani zao hilo linachangia katika pato la Taifa.

2.9 BENKI KUU YA TANZANIA (BOT) - TAWI LA ZANZIBAR

Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa mwaka 1966 kwa sheria ya Benki Kuu iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1965 (The Bank of Tanzani Act of 1965) na kufanyiwa marekebisho mara tatu 1978, 1995 na 2006. Jukumu la msingi la Benki Kuu hiyo ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kutunza thamani ya fedha na kudhibiti mfumko wa bei ili kuchochea ukuaji wa uchumi nchini. Majukumu

mengine yanayotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania Tawi la Zanzibar ni kama ifuatavyo:

a) Kuhifadhi fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na za Benki za Biashara zilizopo Zanzibar.
b) Kufuatilia mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar.
c) Kushiriki katika vikao vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vinavyohusiana na kupanga ukomo wa matumizi ya Serikali (ceiling committee).
d) Kufanya tafiti za kiuchumi kwa ajili ya kutoa ushauri mzuri kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Serikali kwa ujumla wake.
e) Kushirikiana na Taasisi za Serikali ikiwemo Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar kwa kuchangia fedha taslimu kwenye kuandaa ripoti ya ukuaji wa uchumi (GDP) ya robo mwaka (Quarterly Gross Domestic Product Report), ripoti ya maendeleo ya fahirisi za bei kwa mwezi (Consumer Price Index) na taarifa za maendeleo ya sekta ya Viwanda (Quarterly Manufacturing Statistics).
f) Kwa kutumia wataalamu wake, Benki Kuu inaijengea uwezo Tume ya Mipango ili kutengeneza mfumo ambao utawawezesha kubashiri (forecasting) kiwango cha mfumuko wa bei wa Zanzibar.

2.9.1 GAWIO LINALOTOKANA NA MAPATO YA BENKI KUU

Katika utendaji wa shughuli zake, Benki Kuu huzalisha mapato na asilimia 4.5 ya mapato hayo hutolewa kama gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kwa mwaka 2014/2015, SMZ ilipata gawio la Tzs. 5.8 bilioni wakati mwaka 2015/2016, SMZ ilipata gawio la jumla ya shilingi Tzs. 13.5 bilioni na kuzitumia kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo. Hili linadhihirisha wazi kwamba iwapo Benki Kuu inapata mapato katika shughuli zake, utaratibu wa ugawaji wa asilimia ya gawio la Zanzibar huwa inatolewa.

CHANGAMOTO

1. Baadhi ya wananchi kukosa uelewa mzuri wa majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania jambo ambalo hupelekea kufika Ofisini kwa mahitaji ya huduma za kibenki.
2. Wananchi wengi kukosa mwamko juu ya fursa za uwekezaji katika masoko ya fedha nchini.
3. Baadhi ya wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya namna ya kuzitambua noti halali ili kuepuka upokeaji wa noti bandia.
4. Wananchi wengi hupendelea kufanya malipo kwa fedha taslimu jambo ambalo linaongeza uchakavu wa noti na kuisababishia hasara Benki Kuu ya kuchapisha noti mpya. Aidha, matumizi ya fedha nyingi hususan kwa Wafanyabiashara wakubwa huhatarisha usalama wao kutokana na wahalifu.
5. Baadhi ya benki za biashara kushindwa kufikia viwango vya ubora vilivyowekwa na Benki Kuu na kupelekea kufungwa kwa benki hizo na kusababisha usumbufu kwa Wananchi.
6. Kuwepo kwa uelewa mdogo kwa wananchi kuhusu uhifadhi wa fedha zao Benki na kuamua kuzihifadhi kwa njia za kienyeji na kupelekea kuharibika kwa fedha hizo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ingawa huduma za Benki Kuu zinatolewa Kisiwani Pemba kupitia kituo chake kilichopo ndani ya jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) - Chakechake, Kamati inaitaka BOT ianzishe jengo la Ofisi yake huko Pemba ili kuwapa fursa zaidi wananchi kufaidika na huduma za Benki Kuu moja kwa moja pamoja na wananchi wetu kuwa na uelewa wa kuwepo Benki hiyo.
2. BOT iweke utaratibu wa kutumia vyombo vya habari vikiwemo ZBC Redio na Televisheni ili wananchi wajue majukumu wanayoyatekeleza.
3. Benki Kuu itafute utaratibu wa kuyashughulikia mapato yanayofanyika kupitia miamala ya simu.

2.10 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

2.10. 1 TAWI LA CHAKECHAKE NA MKOANI

Kamati ilipata fursa ya kutembelea kituo cha Benki ya Watu wa Zanzibar Tawi la Chakechake na kituo cha huduma cha Mkoani Pemba ambavyo vinatoa huduma zote za Kibenki (Islamic and conventional Banking). Kwa upande wa Tawi la Chakechake Pemba, ambalo ni miongoni mwa Matawi makongwe yaliyoanzishwa mwaka 1966. Tawi hilo lina vituo viwili vya kutolea huduma (Service centre) vya Wete na Mkoani na mashine nne za kutolea fedha.

CHANGAMOTO

1. Kukosekana kwa uzio katika kituo cha Mkoani.
2. Kituo cha Mkoani kinakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na usafiri kwa Watendaji wake.
3. Kituo cha Mkoani hakina usawa wa kijinsia kwani wafanyakazi wote wa kituo hicho walikuwa wanaume.
4. Mwamko mdogo walionao wananchi juu ya umuhimu wa kuhifadhi fedha za mauzo ya karafuu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Benki ijipange kutoa mikopo kwa wananchi wa kawaida na sio kuwapatia mikopo Wafanyakazi wa Serikali na Taasisi zake tu kwani Kamati imebaini kuwa wananchi walio wengi si waajiriwa wa Serikali na pia wanahitaji mikopo nafuu kwa ajili ya kujikwamua na hali ya umasikini.
2. Kamati inawasisitiza Watendaji Wakuu wa Kituo cha PBZ Mkoani kumaliza ujenzi unaoendelea ndani ya wakati uliopangwa ili kukidhi vigezo vya kibenki na kurahisisha huduma kwa wananchi wa Mkoani na Vitongoji vyake.
3. PBZ izidi kutoa uelewa kwa Wakulima na Wananchi wetu ili wahamasike kuweka pesa zao Benki hususan katika kipindi cha msimu wa uchumaji wa karafuu.
4. Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) iharakishe kutoa huduma kwa njia ya Uwakala ambayo itapunguza msongomano wa wateja pamoja na kutoa ajira kwa wananchi hususan vijana.

5. PBZ ihakikishe kituo cha Mkoani kinazungushiwa ukuta ili kupata hifadhi inayostahiki.

2.11 BENKI YA CRDB

Benki ya CRDB ni kati ya benki binafsi ambayo imefungua Tawi lake hapa Zanzibar kwa lengo la kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa wananchi wetu. Miongoni mwa huduma zinazotolea na Benki hiyo inajumuisha kuwakusanya wakulima na kuwataka walime kisasa kwa njia ya 'green house'. Aidha, wanawakopesha watu wa kati (Middleman) ili kuweza kununua bidhaa kwa wakulima. Mbinu wanayotumia ni kuwakusanya wazalishaji (wakulima) kimajimbo na kuwawezesha ambapo kila mkulima atalazimika kuchangia katika jumuiya yao. Utaratibu huu unaitwa 'Value Chain' na tayari umeanza kutumika katika maeneo ya Kiuyu Pemba kwa wazalishaji wa Chumvi.

CHANGAMOTO

Wateja wengi wa Benki hiyo huwa wanatoka Tanzania Bara ambao hutakiwa kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ili waweze kufungua 'account' kama zinavyotaka taratibu za Benki. Hivyo, wanapendekeza itumike barua ya sheha kuthibitisha ukaazi na utambulisho wake.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kupitia Mpango wa kuwainua wajasiriamali wadogowadogo (Micro finance entrepreneur), Kamati inaiomba benki ya CRDB kuwapatia mikopo nafuu Wajasiriamali ambao wamejiwekeza katika sekta mbalimbali.

2.12 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA

Mamlaka imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016, ikiwa na dhima kuu ya kusimamia utaratibu mzima wa ununuzi na uondoshaji wa mali katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha (value for money) katika ununuzi na uondoshaji wa bidhaa na utoaji huduma za umma pamoja na kuimarisha uchumi katika sekta hiyo.

Hadi Kamati inaitembelea Mamlaka hiyo mpya tayari ilikuwa imeshafanya vikao vya kujadili Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, vikao vya kuwatambulisha wakuu wa vitengo vya ununuzi na uondoaji wa mali za umma, ununuzi wa vifaa vya Ofisi, kuunda muundo wa Mamlaka (organization structure) na kuanza kazi za kawaida za Ofisi.

CHANGAMOTO

1. Udogo wa eneo wanalolitumia kwa shughuli za Ofisi kwani Kamati ilishuhudia watendaji wa Mamlaka wakiwa wamejibana kwenye jengo la Uwekezaji la Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) liliopo Kinizini.
2. Kuchelewa kufanyika uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka kunakwamisha utoaji wa maamuzi juu ya mambo ya msingi ya utendaji wa shughuli zake.
3. Ukosefu wa vyombo vya usafiri ni tatizo sugu kwa Mamlaka kwani Mamlaka haina gari kwa ajili ya shughuli za Ofisi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha inaipatia gari Mamlaka itakayorahisisha shughuli za kila siku za Mamlaka.
2. Mamlaka itoe uelewa kwa Taasisi za Serikali na binafsi ambazo zinafanya manunuzi au kutoa huduma katika Taasisi za Seikali. Hali hiyo itaziwezesha Taasisi hizo kufuata Sheria na Kanuni za Manunuzi nchini.

2.13 SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR - TAWI LA PEMBA

Kamati ilitembelea eneo jipya linalotarajiwa kujengwa Ofisi ya kudumu ya Shirika la Bima la Zanzibar katika Mji wa Chakechake na kukuta kiwanja kimeshasafishwa vizuri ili kupisha ujenzi wa jengo la kisasa la Shirika kwa upande wa Pemba. Kwa sasa kiwanja hicho kinatumiwa na wafanyabiashara wadogo wadogo hadi hapo shughuli za ujenzi zitakapoanza rasmi. Kamati ilielezwa kuwa hapo awali eneo hilo lilikuwa na jengo chakavu lililokuwa likimilikiwa na Wizara inayoshughulikia Ardhi - Pemba na kufanikiwa kulibomoa kwa kutumia kampuni ya TK. Engeneering kwa gharama ya 35,973,000 milioni.

CHANGAMOTO

1. Kuchelewa kupata ufumbuzi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango juu ya kandarasi ya ujenzi wa jengo la Bima Pemba.
2. Kutokuwepo kwa usiri wa vikao vya kiutendaji vinavyotoa maamuzi mbalimbali.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Shirika lihakikishe linamsimamia vyema Mkandarasi wa ujenzi ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha ‘value for money’ inakuwepo kwenye jengo hilo na kunusuru matumizi mabaya ya fedha za Serikali.
2. Kamati inashauri kuwepo na usiri wa vikao vya kiutendaji ili siri zihifadhike na asiyehusika asipate mwanya kuingilia masuala ya Ofisi.
3. Kamati inaitaka Wizara kupitia Shirika la Bima la Zanzibar kufuata kikamilifu taratibu za uondoshaji wa mali za Serikali kwani hata kama vifaa vimeharibika basi Wizara inajukumu la kuviwasilisha vifaa hivyo Wizara ya Fedha na Mipango kwa utaratibu wa “Zero disposal” kama inavyoelekezwa na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

2.14 SHIRIKA LA BIMA - TAWI LA MWANZA

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kushirikiana na Shirika la Bima la Zanzibar ilifanya ziara ya siku tatu Jijini Mwanza kuanzia tarehe 22 Agosti hadi tarehe 24 Agosti, 2017. Lengo la ziara ilikuwa ni kuhudhuria na kushiriki katika hafla maalum ya uhamasishaji wafanyabiashara hususan waliopo Mwanza kukata Bima za biashara na mali zao kupitia Shirika la Bima la Zanzibar.

Wajumbe wa Kamati waliwaelimisha washiriki wa hafla hiyo juu ya umuhimu wa kukata bima zao kwenye Shirika la Bima la Zanzibar na kuwaomba wawe mabalozi wazuri watakapoondoka hapo kwa kuwashajhisha wafanyabiashara wengine wawe na utamaduni wa kukata Bima hususan kupitia shirika la Bima la Zanzibar ambalo limeenea Tanzania nzima, wanaaminika na vilevile ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenye uzoefu wa siku nyingi katika masuala ya Bima na wala haina ubabaishaji.

CHANGAMOTO

Kutozwa kwa asilimia 18 ya VAT na ZRB kwa wateja wao. Suala hili linapelekea gharama za bima kuwa kubwa na kuwafanya wateja wengi wasishawishike kujiunga na shirika hilo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia upya suala la kodi ya asilimia 18 ya VAT kwani inafanya gharama za bima kuwa kubwa mno.
2. Wizara ihamasishe wananchi kukata bima zao kwenye Shirika la Bima la Zanzibar ili Shirika liendelee kutengeneza faida.

SEHEMU YA TATU

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Idara nne, Shirika moja, Baraza moja pamoja na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

i. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
ii. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
iii. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko;
iv. Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali;
v. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC);
vi. Baraza la Usimamizi wa Utoaji Leseni;
vii. Shirika la Viwango la Zanzibar (ZBS);
viii. Baraza la Taifa la Biashara;
ix. Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (PBRA); na
x. Afisi Kuu - Pemba.

3.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Tzs. 7,210,202,000 bilioni. Kati ya fedha hizo, Tzs. 4,460,200,000 bilionii ni kwa ajili ya kazi za kawaida na Tzs. 2,750,000,000 bilioni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Disemba 2017, Wizara iliomba jumla ya Tzs. 3,787,835,896 bilioni na kupatiwa jumla ya Tzs. 2,289,700,482 bilioni sawa na asilimia 54 ya fedha ilizoomba. Aidha, Wizara kupitia vyanzo vyake mbalimbali vikiwemo vipimo na mizani, usajili wa Makampuni na kazi za biashara ambapo hadi kufikia Disemba 2017, Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs. 236,201,769 milioni na imefanikiwa kukusanya Jumla ya Tzs. 621,897,246 milioni sawa na asilimia 263 ya makadirio ya makusanyo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba kama inavyoonekana katika Jadueli hapa chini.

Jadueli Namba 2: Makusanyo ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2017

Nam.	Maelezo ya mapato	Makadirio ya makusanyo	Makusanyo halisi	%ya makusanyo
1.	Vipimo na Mizani	49,300,000	24,448,963	50%
2.	Kazi za Biashara	36,060,000	279,651,763	776%
3.	Ada utunzaji urithi	82,000	0	0%
4.	Alama za Biashara	70,399,000	57,137,600	81%
5.	Uandikishaji Makampuni	43,195,000	102,112,020	236%
6.	Uandikishaji majina ya Biashara	18,381,100	22,855,500	124%

7.	Ujira wa kutengeneza nyaraka	18,784,669	52,552,300	280%
8.	Mapato mengine ZRB 18 na Stamp	0	83,139,100	
	JUMLA KUU	**236,201,769**	**621,897,246**	**263%**

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kufuatia ukusanyaji huo wa miezi sita uliovuka lengo, kamati inaipongeza Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na kuitaka isibweteke na mafanikio yaliyopatikana na badala yake iongeze juhudi katika kuvisimamia ipasavyo vyanzo vyake vya mapato na kuongeza zaidi makusanyo ifikapo mwisho wa mwaka. Kimsingi, Kamati imeridhishwa na utendaji wa Wizara na kuiomba iwe makini katika ukusanyaji wa takwimu zake hususan takwimu za hali ya upatikanaji wa chakula nchini ili kuhakikisha zinakua sahihi na kuifanya mipango ya Serikali kuwa ya uhakika zaidi. Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kusimamia imara ukodishwaji wa zao la karafuu katika msimu huu na kupelekea kuongezeka maradufu kwa mapato ya Serikali.

CHANGAMOTO

1. Kumekuwa na ongezeko kubwa la hadaa za kibiashara nchini jambo ambalo linarudisha nyuma wafanyabiashara wadogo wadogo na ni kinyume na mila, utamaduni na silka zetu.
2. Ingawa biashara ya dagaa ni yenye tija kubwa kwa wanachi wetu, bado inakabiliwa na tatizo la kukosa usimamizi wa vyombo vinavyohusika. Hivyo, kupelekea wajanja wachache kufaidika zaidi kupitia nguvu za wananchi wetu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wafanyabiashara wote watakaobainika wanauza bidhaa zilizopitwa na wakati wa matumizi yake ili kuwalinda wananchi wetu na madhara makubwa yanayoweza kuwapata kutokana na matumizi ya vyakula vilivyopitwa na wakati.
2. Kamati inaishauri Wizara kuwaelimisha Wajasiriamali kutumia fursa za maonyesho yanayofanyika katika Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar za kila mwaka, siku ya Wakulima Sabasaba - Dar es Salaam na yanayofanyika nje ya nchi.
3. Wizara iiweke utaratibu mzuri wa uendeshaji wa biashara ya dagaa kwa upana wake kwani inatoa ajira kwa wananchi wengi na ni biashara yenye tija.

3.2 SHIRIKA LA TAIFA LA BIASHARA (ZSTC)

3.2.1 FIDIA YA WAHANGA WA KARAFUU

Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kupitia (ZSTC) kwa kuwafariji wananchi ambao walipata ajali mbalimbali kutokana na harakati za kuliokoa zao la karafuu. Miongoni mwa faraja hizo ni kuwapatia kifutajasho ambacho husaidia kwa kiasi kikubwa matibabu ya wahanga hao.

CHANGAMOTO

1. Udhibiti mdogo wa watoto chini ya miaka 18 kujihusisha na uchumaji wa zao la karafuu na kupata athari mbalimbali.
2. Ukosefu wa elimu juu ya taratibu za kufuatwa hadi mwananchi kupatiwa kifuta jasho (fidia) baada ya kuanguka katika mikarafuu nalo ni tatizo kwani baadhi ya waathirika hubaki wakisononeka tu bila ya kupata msaada wowote.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iangalie upya viwango vya malipo ya kifutajasho kwani imebainika kuwa viwango hivyo ni vya muda mrefu na haviendi na wakati uliopo na dhamira ya dhati ya Serikali kuwasaidia wananchi wake waliofikwa na majanga hayo.
2. Kamati inawaomba wananchi wasivunjike moyo bali waendelee na juhudi za kuliokoa zao letu la Taifa kwani ajali humfika mtu yeyote kwa wakati wowote.
3. Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara iandae mafunzo ya namna ya uchumaji bora wa karafuu kwa wananchi ili kuwaepusha na ajali.
4. Kamati inaisisitiza ZSTC kufanya utafiti wa kugundua fedha zinazotolewa na PBZ kulikopesha Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wa karafuu ziko kwenye mzunguko wa fedha na mwishowe zinarudi Benki ya Watu wa Zanzibar kwa matumizi mengine.

3.2.2 ZIARA YA KAMATI - DUBAI

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya ziara ya siku nne nchini Dubai mnamo tarehe 03 Julai, 2017 hadi tarehe 06 Julai, 2017. Lengo kuu la ziara ilikuwa ni kufuatilia utendaji kazi wa Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) pamoja na Shirika la Biashara la Taifa la Zanzibar (ZSTC). Kamati ilikutana na watendaji wa Kampuni ya "Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech." iliyopo Sharjah ambayo imeingia Mkataba na Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) mwaka 2006 kushughulikia ukaguzi wa ubora na viwango vya magari yanayonunuliwa na wafanyabiashara nchini Dubai kabla ya kusafirishwa kuletwa Zanzibar.

Kamati pia ilishuhudia mashine mbali mbali zinazomilikiwa na Kampuni ya Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech. ambazo hutumika kupimia "Brake", "Side Slip Tester", "Shock Absorber Tester" na "Petrol Smoke Tester" kama zinavyoonekana katika Jadueli hapa chini.

Jedueli Namba 3: Vifaa vya kampuni ya Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech.

SL. NO.	MESHINE NO.	NAME OF MACHINE	QUALITY
JK/001	S/L:B-404059	BRAKE TESTER	1
JK/002	S/L:431559-001	SHOCK OBSORBER	1
JK/003-01		LIGHTER TESTER	1
JK/004-01	S/L:07930001	PETROL SMOKE TESTER	1
JK/004-02	P/N898GOMB/KP3	PETROL SMOKE TESTER (PETROL AND DIESEL)	1
JK/014	S/L:451943-001	SIDE SLIDE TESTER	1
JK/007	Z00000471	ENGINE SCANNER	1
JK/010	H13080132	WHEEL ALIGNMENT	1
JK/011-01, JK/011-02	SL1320	DIGITAL SOUND TESTER	2
JK/013-01,JK/013-02	31991	RADIATION SCANNER	2
JK/003-02	140349	LUMINATOR/LIGHT TESTER	1
JK/005-01	L6108	SCISSOR LIFT 4 TONS	1
JK/005-02	5.2251E+11	SCISSOR LIFT 2 TONS	1
JK/006	-	BATTERY BOSTER	1
JK/008	ATB1301	BATTERY BOSTER	1
JK/009	3495770011	AIR COMPRESSOR	1
JK/012	QL-3100CB	WATER PRESSURE WASHER	1
JK/015	-	TIRE GROOVE TESTER	1
JK/016	GV-15HS	OIL DISPENSER	2
JK/017	-	VERNIER CALIPER	1

Chanzo: kampuni ya Jabal Kilimanjoro

Aidha, Kampuni hiyo ina Mkataba halali iliyoingia na Taasisi ya Viwango Zanzibar pamoja na usajili wa kufanya kazi iliyokusudiwa. Sambamba na hayo, Kampuni inamiliki eneo, vifaa vizima na vya kutosha kufanyia kazi zake pamoja na Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo kwani Kamati imebahatika kujionea vyeti vya mafunzo waliopatiwa wafanyakazi hao.

CHANGAMOTO

1. Kutopitishwa kwa magari katika Kampuni hiyo kwa ajili ya kukaguliwa kunakofanywa na baadhi ya Wafanyabiashara wajanja.
2. Kuingia na kupokelewa kwa magari katika Bandari ya Zanzibar yaliyokuwa hayajakaguliwa licha ya kufahamika kuwa Serikali imeingia mkataba na Kampuni hiyo katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ubora wa magari yanayoingia Zanzibar.
3. ZBS kushindwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kujionea wenyewe Kampuni ya 'Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech.' inavyofanyakazi kwa mujibu wa mkataba.
4. ZBS kutopata mashirikiano ya kutosha kutoka Taasisi nyengine za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kuwadhbiti wanaokwepa kukaguliwa hususan wanaoingiza bidhaa Zanzibar bila ya kufanyiwa ukaguzi nje ya Zanzibar.
5. Kutokaguliwa mara kwa mara kwa kampuni za ukaguzi za Dubai na Japan.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara kwa kushirikiana na Kamati ifanye ziara nchini Japan kwani imeonekana changamoto za ukaguzi wa ubora wa viwango vya magari zinatokea zaidi huko Japan.
2. Wizara ihakikishe kunakuwepo mashirikiano ya wazi na utaratibu maalum kati ya Shirika la Bandari la Zanzibar, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) kuhusu ukaguzi wa magari.
3. Kuwepo utaratibu maalum utakaoiwezesha Kampuni ya 'Jabal Kilimanjaro Auto Elect. Mech.' kuwasilisha taarifa za kiutendaji kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Viwango, Katibu Mkuu na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.
4. Wizara ihakikishe Kampuni na Taasisi ya Viwango Zanzibar zinaandaa mafunzo kwa Kampuni za usafirishaji magari kuhusu athari ya kusafirisha magari pasi na kufanyiwa ukaguzi.
5. Wizara ihakikishe kunakuwepo "One Stop Center" itakayokuwa inashughulikia malipo ya ukaguzi wa magari na baadhi ya bidhaa nyengine hapo Bandarini Zanzibar.
6. Kamati inaisisitiza Wizara kuandaa mipango madhubuti itakayowatia hatiani wale wote wanaosafirisha magari bila ya kuwa na cheti cha ukaguzi kinachotambulika na SMZ.
7. Magari yaliyogundulika kutofanyiwa ukaguzi nje ya nchi yafanyiwe ukaguzi yakifika Zanzibar.

3.2.3 TAWI LA BIASHARA ZA KIMATAIFA NCHINI DUBAI

Mnamo tarehe 05 Julai 2017, Kamati ilifanya ziara katika Tawi la Biashara ya Kimataifa nchini Dubai ambalo kiutendaji linasimamiwa na Idara ya Masoko ya ZSTC. Kamati ilielezwa kwamba Tawi hilo lilianzishwa April, 1993 katika eneo la "Carboad" karibu na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Dubai na baadae likahamishiwa katika eneo la Viwanda lijulikanalo "Alghusais Industrial Area No. 1" likiwa katika "warehouse" no. E-13. Kiutendaji Tawi hilo lina Wafanyakazi watatu kutoka nchini India wakiwemo Mhasibu, Mhudumu na Dereva pamoja na Mfanyakazi mmoja ambae huwa anaajiriwa kwa muda kwa ajili ya kutafuta masoko katika kipindi ambacho karafuu zimeingizwa ghalani.

CHANGAMOTO

1. Kusinyaa kwa karafuu kutokana na hali ya hewa ya joto kali na kupoteza uzito na ubora wake.
2. Kuwepo juu gharama za uendeshaji wa Tawi hilo.
3. Kutokuwepo Mfanyakazi mzalendo kutoka Zanzibar alieajiriwa maalum kufanya shughuli za uendeshaji wa Tawi hilo huko Dubai.
4. Wizara iendelee zaidi kutafuta masoko kwani hadi sasa Tani za karafuu zinazopelekwa Dubai ni kidogo ukilinganisha na zile zinazobakia Zanzibar.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ifanye utafiti wa kuangalia gharama za uendeshaji wa Tawi hilo kwani inaonekana ni kubwa.
2. Kamati inaishauri Wizara iajiri mfanyakazi Mzawa kutoka Zanzibar ambae ndie awe Msimamizi Mkuu wa Tawi hilo.
3. Ufanyike ukaguzi wa mara kwa mara katika Tawi hilo ili kubaini haraka pale yanapotokea mapungufu na kuyatatua kwa haraka.
4. Wizara ifungue Matawi zaidi katika nchi nyengine zinazotumia karafuu kwa wingi kama vile India iwapo utafiti utakaofanywa utaonesha kama kuna haja ya kuwa na Matawi hayo kwa ajili ya kukuza biashara ya karafuu.
5. Shirika lijitangaze zaidi katika kutafuta masoko ya Karafuu.
6. Kamati inaitaka Wizara kupitia Shirika la ZSTC liangalie uwezekano wa kuhamasisha ulimaji, usafirishaji na uuzaji wa bidhaa za viungo kama vile Hiliki, Mdalasini na pilipili manga ili kuongeza pato la Taifa na kuondoa umasikini.
7. Kitengo cha Masoko cha ZSTC kiajiri wafanyakazi waliobobea katika fani na utaalamu wa Masoko ili kuzitangaza karafuu na bidhaa nyengine zinazozalishwa Zanzibar.
8. Kufanyike utafiti wa ubora wa karafuu za Zanzibar ukilinganisha na zile za nchi nyengine.
9. Kamati inasisitiza kuwa ritani za mauzo ya karafuu Dubai ziwe zinawasilishwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

3.2.4 TAWI LA ZSTC - DAR ES SALAAM

Kufuatia kufanyika kwa ziara ya siku nne ya kikazi katika Tawi la ZSTC nchini Dubai, Kamati iligundua kwamba ipo haja ya kuyatembelea Matawi au Vituo vyengine vya ZSTC viliopo ndani na nje ya Zanzibar ili kupata tathmini ya faida, hasara na mchango wake kwa maendeleo ya Taifa letu. Kitendo hiki kitaiwezesha Kamati kupata fursa nzuri ya kuishauri Serikali ipasavyo.

Tawi la ZSTC liliopo Dar es Salaam ni Tawi la kihistoria lililoanza mwaka 1972 kwa lengo la kukidhi haja ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kuweza kupatikana Dar es Salaam na kurahisisha uagizaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara. Uwepo wa Tawi hili ni rasilimali kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwani linaashiria mafanikio ya Muungano wa nchi zetu mbili za Tanganyika na Zanzibar. Aidha, kwa kujua umuhimu uliopo katika Tawi hilo, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilifanya ziara ya siku moja katika Tawi la ZSTC tarehe 26 Julai, 2017.

CHANGAMOTO

1. Tawi halina umiliki wa nyumba inayoitumia kwani nyumba wanayotumia inamilikiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).
2. Ukumbi wa mkutano ni mdogo sana ambao haukidhi mahitaji ya shughuli za Tawi hilo.

3. Nyumba inayomilikiwa na Tawi hilo iliyopo maeneo ya Sinza ni chakavu mno na huingia maji ya mvua kutokana na majirani kunyanyua misingi ya nyumba zao.
4. Gharama za uendeshaji wa Tawi hilo ni kubwa zinazopelekea baadhi ya wakati Tawi kupata hasara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inalishauri Tawi kuyapanga vizuri maghala yake ili yaweze kuingiza bidhaa nyingi zaidi na kutumia rasilimali chache kwa kupata faida,
2. Tawi liwatumie Wafanyakazi walionao kuzitangaza bidhaa wanazozalisha na wanazouza.
3. Ili kuokoa fedha nyingi zinazolipiwa kodi ya jengo hilo, Kamati inaitaka Wizara kuendelea kulifuatilia suala la umiliki wa Jengo wanalolitumia na kukifuatilia kiwanja kiliopo karibu na nyumba yao Sinza kwa kukutana na mmiliki wa kiwanja hicho ili waweze kukinunua na kukitumia kwa shughuli za uwekezaji.
4. ZSTC itafute "brand" yake itakayozitofautisha bidhaa zake na bidhaa nyengine ili waweze kuzuia uchakachuaji wa bidhaa wanazozalisha pamoja na kupata nguvu za kisheria za kuwashitaki wote wanaotumia bidhaa hizo kinyume na utaratibu.
5. Wizara ihakikishe Biashara ya duka inafanywa kwa umakini wa hali ya juu kwani ni rahisi kutokea upotevu wa mali. Hivyo, Kamati inawasihi ZSTC Dar es Salaam kuwa makini katika uendeshaji wa biashara zao.

3.2.5 SHAMBA LA ZSTC - MTAKATA

Kamati ilipata fursa ya kutembelea Shamba la Mtakata ambalo liko chini ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya viungo kama vanilla, Michaichai, Mirehani, Pilipili manga, Mikaratusi dawa na Mikaratusi manukato. Mazao yanayopatikana shambani hapo huwa ni malighafi kwa vyungu vya kupikia mafuta mbalimbali vilivyomo shambani humo.

CHANGAMOTO

1. Mwamko mdogo wa wanajamii juu ya umuhimu wa kulima mazao ya viungo umepelekea baadhi yao kutumia sehemu ya shamba hilo kwa kilimo cha muhogo na mazao mengine ya chakula.
2. Kutokuwa na mipango madhubuti ya matumizi ya shamba hilo katika ulimaji wa mazao ya viungo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ifanye juhudi kuhakikisha shamba hilo linalindwa na hakuna eneo ambalo linachukuliwa na Wananchi au Taasisi bila ya idhini yake. ZSTC ichukue hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa yeyote atakaebainika kwenda kinyume na matumizi stahiki ya eneo hilo.
2. ZSTC iwahamasishe na kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kuzalisha mazao ya viungo kama mchaichai ambao wataalamu wamethibitisha kuwa ni wenye tija nzuri kwenye soko la Kimataifa.

3. Kamati inaitaka Wizara kufanya utafiti ili kujua malighafi inayolimwa shambani hapo inatosheleza mahitaji ya kiwanda.
4. Kamati inaitaka ZSTC kuwa na Mpango Maalum wa kuliendeleza shamba la Mtakata.

3.3 UKAGUZI WA VIPIMO NA MIZANI

Kitengo cha Vipimo na Mizani kinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria nambari 4 ya Vipimo ya Mwaka 1983, ikiwa ni pamoja na uhakiki wa vipimo vyote vinavyohusiana na Biashara hapa Zanzibar zikiwemo Mizani za kupimia bidhaa kutoka kwa wauzaji kwenda kwa wanunuzi, mita za kuuzia mafuta vituoni, mita kubwa ziliopo katika Bohari Kuu za Mafuta (Flow meter) ambazo hutumika kwa kuuzia mafuta kwa jumla kwa kumiminia mafuta kwenye magari ya kusambazia, Uwekaji wa vipimo katika matangi ya kuhifadhia mafuta yaliopo katika Bohari pamoja na Vituoni, Uhakiki wa mizani kubwa (Weigh bridge) ambazo hutumika kwa kupimia uzito wa mizigo unaopakiwa katika magari ya kubebea mizigo, pamoja na kutoa ushauri katika mambo yote yanayohusiana na Vipimo vikiwa vya Biashara pamoja na sekta nyengine zikiwemo za Afya, Ulinzi na Usalama, Teknolojia pamoja na Mazingira.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2017, Idara ya Ukaguzi wa Vipimo na Mizani ilikusanya jumla ya Tzs. 23.7 milioni. Kati ya hizo, Tzs. 18 milioni - Unguja na Tzs. 5.3 milioni - Pemba.

CHANGAMOTO

1. Ingawa watendaji wa Taasisi hii wanafanya kazi kwa uzalendo wa hali ya juu bado vifaa wanavyotumia sio vya kisasa na havikidhi mahitaji ya ukaguzi.
2. Idara inafanya kazi zake za ukaguzi kwa kutumia gari moja ambayo ni chakavu mno na mara kadhaa husindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na ukosefu wa mafuta.
3. Sheria ya Biashara Namba 4 ya mwaka 1983 inayoelekeza majukumu ya Idara hii ni ya zamani mno na inahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa ili iende na wakati.
4. Wakaguzi wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani hadi sasa Baraza la vipimo ambalo ndilo chombo kikuu cha utoaji wa miongozo ya utendaji wa wakaguzi wa vipimo bado halijaundwa. Hali hii inapelekea shughuli za ukaguzi zinazoendeshwa kukosa uhalali wa kisheria.
5. Kukosekana kwa mihuri ya kuthibitisha ukaguzi wa vipimo ni tatizo sugu linalopelekea usumbufu kwa wananchi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuangalia upya muundo wa Idara hii kwani imebainika kuwa hakuna nchi yoyote duniani inayofanya kazi za ukaguzi wa vipimo kwa kupitia Idara kama ilivyo hapa nchini. Hali hii inazorotesha maendeleo ya vipimo na kuhatarisha afya ya mlaji.
2. Wizara iyaangaliwe upya maslahi ya wakaguzi ili kuwalinda dhidi ya ubadhirifu na kurubuniwa na wafanyabiashara.

3. Wizara iandae mfumo bora wa utoaji wa taarifa kwa Idara zake hususan Idara hii ya Ukaguzi kwani Kamati imebaini kuwa ucheleweshaji wa taarifa nao ni kikwazo katikaa utendaji wa wakaguzi wa vipimo nchini.
4. Kamati inaitaka Wizara kusimamia uundwaji wa Baraza la vipimo ili kukidhi matakwa ya sheria na kufanya shughuli za ukaguzi wa vipimo kwa mujibu wa miongozo ya Baraza hilo.
5. Kamati inaishauri Wizara kuandaa lebo maalum itakayobandikwa mara baada ya kukamilika shughuli za ukaguzi kufanyika pamoja na kuwagpngea wateja muhuri.
6. Wizara ihakikishe wa Serikali pamoja na muhuri unaoonesha mwaka wa ukaguzi ili kutekeleza matakwa ya sheria na kuondoa usumbufu wa kukaguliwa mara kwa mara kwa wananchi.
7. Wizara iwawezeshe Wakaguzi wa Vipimo na Mezani kujitangaza kwa njia mbalimbali ikiwemo vipindi vya Redio, Televisheni, Magazeti na hata Mitandao ya kijamiii ili kukuza uelewa wa wananchi kuhusu shughuli za ukaguzi wa vipimo.

3.4 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA)

Wakala wa Usajili Biashara na Mali Zanzibar imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar Namba 13 ya mwaka 2012. Jukumu la msingi la Wakala ni kutoa huduma za usajili wa Taasisi za Biashara na wa Mali kwa wananchi wa Zanzibar na wageni wanaofanya shughuli zao ndani ya Visiwa vya Zanzibar. Wakala tayari imeshaandaa mfumo wa sheria ya usajili wa Taasisi na Mali, Sheria ya Kampuni na sheria ya mfumo wa ufilisi.

Kwasasa Wakala inandaa mfumo wa kusajili biashara (Bussiness Reformation System) kupitia mtandao (online registration) bila ya kufika Ofisini. Aidha, Wakala pia inaendelea na maandalizi ya mfumo wa usajili wa Mali zinazohamishika. Lengo la kuwepo mfumo huo ni kuwasaidia watu waweze kukopesheka kupitia mali zao.

CHANGAMOTO

1. Mgongano uliopo baina ya sheria wanayoitumia na sheria nyengine, mfano Wakala anatakiwa kusajili 'Corporate Society' lakini wao wanasheria yao.
2. Bajeti wanayopatiwa huwa ni ndogo sana ambayo haitoshi kufanikisha malengo waliyojipangia kwani wanashindwa kutoa mwakilishi wa Zanzibar kushiki katika vikao muhimu vya kikazi hasa vile vinavyoandaliwa na "African Regional Intelectual Property Organization" (ARIPO) na World Intellectual Property Organization (WIPO).
3. Wanakimbiwa na wafanyakazi ambao tayari wameshawapatia mafunzo na wameshakuwa na uzoefu wa kazi.
4. Ukosefu wa usafiri kwani Wakala una gari moja tu ya Mkurugenzi Mtendaji ambapo kwa mujibu wa sheria wanahitajika kutembelea na kuzikagua NGO's lakini wanashindwa kutekeleza jukumu hilo.
5. Ufinyu wa nafasi katika Ofisi wanayoitumia pamoja na upungufu wa vitendea kazi na wafanyakazi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iisaidie Wakala kupata mazingira mazuri ya kuendesha shughuli zake za kila siku kwa kutumia sheria yao badala ya sheria ya "corporate society" kama ilivyo hivi sasa.
2. Wizara iisaidie Wakala kwa kuwapatia usafiri na vitendea kazi.
3. Kamati inaitaka Wakala kufuatilia nembo ya Wakala ambayo tayari imewasilishwa Wizarani kwa hatua zaidi ili kuwapa fursa Watendaji kuendelea na shughuli zao kikamilifu.
4. Wizara ifanye juhudi za makusudi kujaza nafasi tupu za Wakala ili kuufanya Wakala uendelee na shughuli zake ipasavyo.

3.5 KIWANDA CHA USHONI CHA IDARA MAALUM ZA SMZ

Kiwanda cha Zanzibar Quality Tailoring Limited (ZQTL) kilichopo eneo la Viwanda Vidogovidogo Amani chini ya usimamizi wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Idara maalum zote.

Kiwanda hiki kilizinduliwa rasmi tarehe 10/01/2005 na Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya sita Mheshimiwa Dk. Amani Abeid Karume, kwa uzinduzi wa mashine za kushonea zenye thamani ya Tzs. 96,000,000 milioni ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Watu wa China. Kiwanda hicho kinaongozwa na Bodi ya Wakurugenzi ambayo ni miongoni mwa Mkuu mmoja kati ya Wakuu wa Vikosi vya SMZ. Aidha, madhumuni makubwa ya uzalishaji ni kujitosheleza kwa ushonaji wa Sare za wapiganaji wa Vikosi vya SMZ na pia kufanya kazi za kibiashara zinapotokezea.

CHANGAMOTO

1. Ukosefu wa mtaji wa kutosha wa kukiwezesha kiwanda hicho kujiendesha kwani kiwanda kilianzishwa mara tu baada ya kupatikana msaada wa mashine kutoka Jamhuri ya Watu wa China.
2. Uhaba wa mashine za kufanyia kazi.
3. Kuwepo kwa deni kubwa linalodaiwa kiwanda hupunguza ufanisi wa shughuli wanazozifanya.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kufanya juhudi za ziada ili kuhakikisha jeshi la Polisi linalipa deni la Tzs. 11 milioni kwa kiwanda hicho.
2. Kiwanda kipatiwe kasma yake kwenye bajeti au kirudishiwe ruzuku ambayo ilikuwa ikipatiwa hapo awali.
3. Kamati inaiomba Serikali ikipatie mtaji Kiwanda hicho kwa ajili ya kununua mashine ambazo zimekosekana ili kiweze kuzalisha nguo bora zitakazokidhi ushindani wa biashara ya ndani na nje ya nchi.
4. Kiwanda kipatiwe maeneo yake ya kufanyia kazi ili kijitanue zaidi na kuzalisha kwa wingi.
5. Kamati inaishauri Wizara kufanya utafiti juu ya namna bora ya kukiendesha kiwanda hicho kibiashara na kuyatekeleza matokeo ya utafiti huo kwa mustakbali mwema wa Vikosi vyetu na Taifa kwa ujumla.

3.6 MAMLAKA YA KUSIMAMIA UZALISHAJI KWA AJILI YA USAFIRISHAJI (EPZA) UBUNGO DAR - ES - SALAAM

Mnamo tarehe 24 Juni 2017, Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo walifanya ziara ya kujifunza kwa kutembelea Mamlaka ya Kusimamia Uzalishaji kwa ajili ya Usafirishaji (Export Processing Zones Authority) (EPZA) yaliyopo Ubungo Jijini Dar-es-sallaam. Lengo kuu la ziara hiyo ilikuwa ni kujifunza namna ya uendelezaji wa maeneo yetu ambayo tumeyatenga kwa ajili ya shughuli za kibiashara kwa wawekezaji na wajasiriamali wadogo wadogo.

Kamati iligundua kwamba ili kufikia Zanzibar ya Viwanda, suala la urithishaji wa taaluma baina ya kizazi kimoja na chengine ni lenye umuhimu wake. Maendeleo ya kweli ya Viwanda hayawezi kufikiwa kwa kizazi kimoja pekee, hivyo mipango madhubuti iandaliwe ikiwemo mitaala inayofaa kwa ajili ya uendelezaji wa hatua za kuelekea uzalishaji na usafirishaji kwenye maeneo yetu.

CHANGAMOTO

1. Kuwepo kwa maeneo mengi Zanzibar ambayo bado hayajaendelezwa.
2. Kutokuwepo kwa vijana wenye elimu ya kutosha katika fani mbali mbali zinazohusiana na uzalishaji, uuzaji na mipango mizima ya Viwanda kwani maendeleo ya viwanda na uwekezaji yanahitaji uwepo wa watu wenye utaalamu tofauti.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Afisi ya Baraza la Wawakilishi iwawezeshe Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kufanya ziara zaidi kwenye viwanda vya kusarifu matunda na viungo vilivyopo Mapinga - Morogoro ili kupata uelewa mpana juu ya masuala ya uwekezaji kwenye maeneo huru ya kiuchumi.
2. Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iangalie uwezekano wa kukanzisha bidhaa za kipekee (unique products) ambazo tutazilinda katika soko kwa kuzifanyia ‘branding’. Kufanya hivyo, kutawavutia wawekezaji mara baada ya kuweka miundo mbinu inayohitajika na itatusaidia kunyanyua kiwango chetu cha usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi na kupelekea ongezeko la fedha za kigeni.
3. Kamati inaiomba Serikali kuwekeza kwenye miundo mbinu ya uhakika ya Bandari pamoja na Viwanja vya ndege vyenye kuhimili kazi za usafirishaji wa biashara.
4. Wizara ijikite katika uanzishwaji wa viwanda ambavyo vitakuwa ni chachu ya kukuwa kwa sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi vikiwemo Viwanda vya maziwa, usindikaji wa matunda na samaki, jamu, juisi ni vya kupewa kipaumbele maalumu kwa nia ya kuongeza ajira kwa vijana wetu.
5. Kamati inaishauri Wizara kuanzisha mashirikiano ya dhati kati ya Tanzania Bara na Zanzibar hususan katika masuala ya uandaaji wa sera na sheria za uwekezaji na uanzishwaji wa Viwanda kwa manufaa ya nchi mbili hizi.

SEHEMU YA NNE
WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni moja kati ya Wizara muhimu zinazosimamiwa kiutendaji na Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ambapo takriban asilimia arubaini ya wananchi wetu wanategemea moja kwa moja kipato chao katika sekta ya kilimo, zaidi ya asilimia hamsini kwa namna moja au nyengine wanategemea sekta ya kilimo kiuchumi na kiasi cha asilimia 25.7 ya pato la nchi yetu limechangiwa na sekta hii muhimu ya kilimo. Kutokana na umuhimu wake, Serikali imewekeza katika sekta hiyo kusaidia kupunguza umasikini katika nchi yetu.

4.1 MUUNDO WA WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hivi karibuni imeongezewa Wakala mbili (Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo na Wakala wa Utafiti wa Mifugo) na Kampuni moja mpya (Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO)); kwa lengo la kuimarisha ufanisi zaidi katika Wizara hiyo. Kwa hivyo, Wizara ina muundo ufuatao:

a) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
b) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
c) Idara ya Kilimo;
d) Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka;
e) Idara ya Umwagiliaji maji;
f) Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe;
g) Idara ya Maendeleo ya Mifugo;
h) Idara ya Maendeleo ya Uvuvi;
i) Taasisi ya Utafiti wa Kilimo;
j) Chuo cha Kilimo Kizimbani;
k) Wakala wa Huduma za Matrekta na zana za kilimo.
l) Wakala wa Utafiti wa Mifugo;
m) Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO); na
n) Ofisi Kuu Pemba.

4.2 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2017, Wizara imepatiwa jumla ya Tzs. 14,028,960,800 billioni ambapo Tzs. 8,707,421,083 bilioni kwa mishahara na Tzs. 3,165,085,742 bilioni kwa kazi za kawaida wakati Tzs. 974,853,975 milioni ni Ruzuku ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo na Wakala wa Matrekta sawa na asilimia 100 ya makadirio na fedha zilizoombwa kwa kipindi cha Julai hadi Disemba. Kwa upande wa fedha za maendeleo hadi kufikia Disemba 30 2017, Wizara imepata Tzs. 2,638,053,212 bilioni ambapo jumla ya Tzs. 1,456,453,212 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Tzs. 1,181,600,000 bilioni kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoombwa kwa kipindi husika.

Katika kusimamia utekelezaji wa bajeti unafanyika kama ilivyopangwa, Kamati imefanya ziara katika maeneo mbalimbali yaliyomo ndani ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ili kuweza kutathmini fedha inayotumiwa inaendana na thamani halisi ya utekelezaji. Katika kuhakikisha hilo linafanyika, Kamati imefanya ziara katika maeneo mbalimbali na kugundua changamoto kadhaa ambazo Kamati imezitolea maagizo yanayohitaji utekelezaji.

4.3 UKODISHAJI WA MASHAMBA YA SERIKALI YA MIKARAFUU PEMBA KWA MSIMU WA MWAKA 2017

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilikabidhiwa orodha ya mashamba ya eka 8,215 kutoka Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ambapo baada ya uhakiki iligundulika mashamba halisi yaliyopo ni eka 8,107. Vilevile, Wizara ilipokea orodha ya mashamba ya eka 2,827 kutoka kwa Masheha na baada ya kuoanisha taarifa hizo za mashamba yatokanayo na madaftari ya Wizara inayoshughulikia Ardhi na zile za mashamba yatokanayo na orodha za Masheha, ilionekana kwamba yapo mashamba 9,982 ambayo baadhi yake yalitolewa mikataba ya eka na mengine hayakuwahi kutolewa mikataba ya aina hiyo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imepewa jukumu la kuyatafuta na kuyakodisha mashamba yote ya Serikali ambayo wamiliki wake hawakupatiwa mikataba ya eka na pia kwa mashamba ambayo wanaostahiki kuyasimamia kwa mujibu wa mikataba ya eka hawapo tena.

Msimu wa mwaka wa 2017 ulikuwa ndio msimu mkubwa kabisa kutokea katika kipindi cha zaidi ya miaka kumi. Karafuu zilizaliwa katika kisiwa chote na ni msimu ulioendelea kwa kipindi kirefu kutokana na wingi wa mvua za masika zilivyokuwa katika kisiwa cha Pemba. Aidha, karafuu zilichelewa kupea kwa vile mara baaada ya mvua za masika kusita jua kali lilitokea mpaka karafuu zikakutana na mvua za vuli. Utaalamu unaonesha kuwa mikarafuu inayozaa katika msimu wa mwaka si aghlabu kuzaa katika msimu wa vuli.

4.3.1 MALENGO YA UKODISHAJI NA UKUSANYAJI MAPATO

Zoezi la ukodishaji lilikuwa na malengo ya kukodisha mashamba ya eka tatu 2,525 kutoka katika Wilaya zote za Pemba ambazo ni Wilaya za Mkoani (683), Chake Chake (255), Wete (537) na Micheweni (50). Aidha, malengo mengine ni kukodisha kwa njia ya zabuni mashamba matano (5) yanayozidi eka tatu kila moja kama yanavyoonekana hapa chini.

Jadueli Namba 4: Eka tano zilizokodishwa kwa Zabuni

NAM.	SHAMBA	WILAYA	SHEHIA
1.	Daya	Wete	Mtambwe Kusini
2.	Vikutani	Wete	Gando
3.	Kinyasini	Wete	Mtambwe Kusini
4.	Kwajini	Mkoani	Mizingani
5.	Makuwe (Ploti Nam. 1 hadi Nam. 10)	Wete	Mgogoni

Chanzo: Ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara ya KMMU

Kwa upande wa mapato, kutokana na kutofanywa tathmini kwa mashamba ya eka tatu, makisio yalifanywa kwa kila shamba kukodishwa kwa wastani wa Tzs. 1,000,000 milioni na hivyo kuwa na makisio ya kukusanya Tzs. 1,525,000,000 bilioni. Aidha, kutokana na tathmini iliyofanywa kwa mashamba makubwa matano ya Serikali yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, makisio ya ukusanyaji wa mapato yalikuwa ni Tzs. 246,803,950 milioni kutoka shamba la Daya Tzs. 3,736,700 milioni; shamba la Vikutani Tzs. 1,803,200 milioni; shamba la Kinyasini Tzs. 15,871,100 milioni; shamba la Kwajini Tzs. 10,629,450 milioni na shamba la Makuwe (Ploti Nam. 1 hadi Nam. 10) 214,763,500 milioni.

Kwa jumla, ukusanyaji wa mapato kutokana na mashamba ya eka tatu na yale yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi yalikisiwa kuwa ni Tzs. 1,771,803,950 bilioni. Hata hivyo, kwa ukaribu wa hesabu Wizara imeweka makisio ya jumla ya Tzs. 2,000,000,000 bilioni kuwa yalitegemewa kukusanywa kutokana na ukodishaji wa mashamba yote ya eka tatu na yale mashamba makubwa yanayozidi eka tatu.

4.3.2 TAASISI ZILIZOSHIRIKI KATIKA UKODISHAJI

Zoezi la ukodishaji wa mashamba ya Serikali liliendeshwa na Kamati Maalum za ukodishaji zilizoundwa na wajumbe kutoka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya, Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA), Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya, Sheha, Bwana/Bibi shamba wa eneo husika pamoja na watu wenye uzoefu wa kuyajua mashamba ya eka kwa kila shehia.

4.3.3 GHARAMA ZA UKODISHAJI

Katika kufanikisha zoezi la ukodishaji kwa msimu wa mwaka wa 2017, jumla ya Tzs. 205,780,000 milioni ziliombwa kwa ajili ya kufanikisha ununuzi wa vifaa vya kazi kama vile vifaa vya kuandikia, mikoba, viatu, myamvuli, mafuta, matangazo, gharama za kikao cha zabuni na posho maalumu kwa wajumbe wote wa kamati ambao walikuwa 57 (22 kwa kamati ya Mkoa wa Kaskazini Pemba na 35 kwa kamati ya Mkoa wa Kusini Pemba).

Hadi kusitishwa kwa zoezi la ukodishaji tarehe 21/09/2017, jumla ya Tzs. 169,436,003 milioni zilipatikana na kutumika kama ilivyokusudiwa. Aidha, Wizara bado inadaiwa jumla ya Tzs. 30,330,200 milioni kwa ajili ya mafuta, posho maalumu na vifaa vya kuandikia. Hali hiyo inafanya gharama ya jumla ya zoezi tokea lilipoanza tarehe 1/7/2017 na kusitishwa tarehe 21/9/2017 kuwa ni Tzs. 199,766,203 milioni.

4.3.4 UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA UKODISHAJI

Zoezi la ukodishaji lilianza kwa kutoa matangazo ya ratiba ya ukodishaji mara tatu kwa muda wa siku tatu mfululizo katika vyombo vya habari vya ZBC Redio na ZBC Televisheni, Zenj FM na Redio Istiqama. Aidha, kikao cha pamoja kati ya wajumbe wote wa kamati za ukodishaji za Mikoa miwili pamoja na Maofisa Wadhamini wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Fedha na Mipango kilifanyika katika ukumbi wa mikutano wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi uliopo Limbani, Wete kwa lengo la kuwapatia wajumbe wa kamati ratiba, utaratibu, maelekezo na nasaha juu ya ufanikishaji wa zoezi la ukodishaji wa mashamba ya karafuu ya Serikali kwa lengo kuu la kukusanya mapato ya Serikali kwa ufanisi mkubwa na kudhibiti magendo ya karafuu.

4.3.5 MATOKEO YA UKODISHAJI NA UKUSANYAJI MAPATO

4.3.5.1 Ukodishaji wa Mashamba ya Eka Tatu

Ukodishaji ulianza tarehe 1/7/2017 na kuendelea hadi 12/8/2017 katika wilaya za Wete na Mkoani kwa awamu ya kwanza ambapo uzinduzi ulifanyika katika Shehia ya Mjimbini. Uzinduzi huo ulifanywa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed ambae ndie Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar. Katika Ukodishaji wa msimu wa mwaka 2017, kamati mbili zilianzishwa, moja ikafanyakazi Mkoa wa Kaskazini na ya pili Mkoa wa Kusini Pemba. Aidha, kwa awamu ya pili ukodishaji ulianza tarehe 15/8/2017 hadi tarehe 21/9/2017 kwa Wilaya za Micheweni na Chake Chake.

Kamati zimefanikiwa kukodisha jumla ya mashamba ya eka 1,452 sawa na asilimia 95 yakiwemo mashamba 543 ya Wilaya ya Wete, 169 ya Wilaya ya Micheweni, 480 ya Wilaya ya Mkoani na 260 ya Wilaya ya Chake Chake. Kati ya mashamba 1,452 yaliyokodishwa, mashamba 553 yalikodiwa na wananchi wanaoyasimamia. Aidha, mashamba 1,062 kati ya mashamba yaliyokodishwa ni sehemu ya orodha ya mashamba yalikuwa kwenye malengo, na mashamba 390 ni mapya yameibuliwa. Muhtasari wa utekelezaji huo ni kama inavyuofuata hapa chini kwenye jedueli:-

Jedueli Namba 5: Muhtasari wa ukodishaji wa mashamba ya eka tatu.

Kundi la mashamba	Mkoani	Chake	Wete	Michweni	Jumla
Mashamba yaliyokodishwa	480	260	543	169	1,452
Mashamba walioyakodi wakulima wanao yasimamamia	200	131	161	61	553
Mashamba yaliyotoka kwenye orodha ya mashamba ya eka yanayokodishika	391	181	442	48	1,062
Mashamba yaliyoibuliwa	89	79	101	121	390

Chanzo: Ofisi ya Afisa Mdhamini wa WKMMU

Jumla ya mashamba 463 yaliyoko kwenye kitini cha mashamba yanayokodishika hayakukodishwa kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo baadhi ya wamiliki walikuwa wanamiliki mikataba ya eka, kuwepo vizuka na mapori na yenye mikarafuu midogo ambayo haijawa tayari kuzaa.

Katika ukodishaji huo, mikataba iliyozingatiwa kuwa ni halali ni ile iliyotolewa na kusainiwa na Waheshimiwa Mzee Abeid Aman Karume na Mzee Aboud Jumbe Mwinyi. Aidha, Wizara imepata taarifa za ukodishwaji wa mashamba 51 kwa Taasisi nyengine yakiwemo mashamba 23 kwa Jeshi la Wananchi Tanzania kambi ya Makuwe, 22 kwa Wakfu na Mali ya Amana, moja kwa Jeshi la Polisi kituo cha Matangatuani, mawili kwa Mahkama na matatu kwa Skuli. Mashamba haya hayakuwemo katika kitini cha Wizara cha mashamba yanayokodishika.

4.3.5.2 Ukodishaji wa Mashamba Makubwa

Mashamba makubwa ya Serikali yaani Makuwe, Daya - Mtambwe, Kinyasini - Mtambwe na Gando - Vikutani yalikodishwa kwa njia ya zabuni. Matangazo ya zabuni yalitolewa kupitia ZBC Redio na TV. Hatimae zabuni zilifunguliwa na Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi mbele ya Wazabuni siku ya tarehe 2 Agosti 2017, saa 8.00 mchana katika jengo la Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Maruhubi Zanzibar. Aidha, jumla ya barua 113 za maombi ziliwasilishwa Bodi ya Zabuni

4.3.5.3 Ukusanyaji wa Mapato

Hadi kufikia usitishaji wa zoezi la ukodishaji, jumla ya Tzs. 2,397,626,000 bilioni zimekodishiwa mashamba na hivyo zinategemewa kukusanywa na Serikali. Fedha hizo zinatokana na ukodishaji wa mashamba ya eka tatu Tzs. 2,072,326,000 bilioni na ukodishaji wa mashamba yanayosimamiwa na Wizara ya Kilimo yaliyokodishwa kwa zabuni Tzs. 325,300,000 milioni. Katika fedha za mashamba ya eka tatu, Tzs. 777,010,000 milioni zimetoka Mkoani, Tzs. 500,380,000 milioni Chake, Tzs. 589,641,000 milioni Wete na Tzs. 205,295,000 milioni Micheweni.

Aidha, hadi kufikia tarehe 19 Januari 2018, jumla ya Tzs. 1,243,048,100 bilioni sawa na asilimia 52 ya mategemeo ya jumla zimekusanywa. Juhudi zinazoendelea kufanywa katika kuhakikisha fedha hizi zinalipwa ni pamoja na kutoa matangazo kwenye redio, kufanya vikao na Wakuu wa Wilaya, Mikoa pamoja na waliokodi mashamba ili kuhakikisha kuwa wamelipa madeni yao.

Aidha, hatua zinazoendelea ili kuhakikisha madeni haya yanalipwa yote ni pamoja na kuorodhesha watu wote waliokodishwa na bado hawajamaliza kulipa kiwango cha deni lao na kuwapeleka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) kwa hatua za kisheria. Kutokana na kasoro mbalimbali zilizojitokeza wakati wa zoezi la ukodishaji, uhakiki wa kupata mapato halisi yanayotegemewa na vifutajasho unaendelea kwa muongozo wa Kamati ya Mawaziri.

4.4 MALIPO YA FEDHA INAYOTOKANA NA HUDUMA YA SHAMBA (VIFUTAJASHO)

Katika zoezi la Ukodishaji watu wanaoyasimamia mashamba wanapaswa kupewa kifutajasho kulingana na vigezo vilivyowekwa na kamati ya ukodishaji. Vigezo hivyo ni kama vilivyoainishwa katika judueli hapa chini:

Jadweli Namba 6: Vigezo vya Malipo ya Huduma ya Shamba (Kifutajasho)

Nam.	Kigezo	% ya Malipo
1	Shamba lililosafishwa ndani ya mwaka husika na kuendelezwa kwa kupandwa mikarafuu na miti mengine ya kudumu.	40%
2	Shamba lililosafishwa ndani ya mwaka husika lakini halikupandwa miti ya kudumu.	30%
3	Shamba ambalo limesafishwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita.	20%
4	Shamba lisilosafishwa na halijapandwa miti lakini anailinda miti iliyomo.	10%

Chanzo: Ofisi ya Afisa Mdhamini WKMMU.

Jumla ya Tzs. 528,309,600 milioni zinatarajiwa kulipiwa kifutajasho kwa wahudumiaji wa mashamba ya eka katika Wilaya nne za Pemba katika ukodishaji wa msimu wa mwaka 2017 zikiwemo Tzs. 148,456,600 milioni Wete, Tzs. 56,074,000 milioni Michweni, Tzs. 191,372,000 milioni Mkoani, na Tzs. 132,407,000 milioni Chake. Aidha, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Ofisi Kuu Pemba tayari imewasilisha maombi ya malipo hayo Wizara ya Fedha na Mipango Ofisi Kuu Pemba.

CHANGAMOTO

1. Baadhi ya Masheha kutoyajua mashamba kwa kukosa mashirikiano na masheha waliowatangulia kwa kutowaonesha mashamba hayo.
2. Uelewa mdogo wa jamii juu ya umiliki wa mashamba hayo
3. Uchelewaji wa malipo ya kodi ya mashamba kutokana na ukosefu wa mzunguko wa fedha. Uzoefu unaonesha kuwa ukodishaji unafanyika wiki moja kabla ya kuanza mavuno ya karafuu. Hivyo, uuzaji hufanyika na wakati huo huo ulipaji hufanywa kwa wakati uliopangwa. kutokana na wingi wa mashamba hayo, ukodishaji umefanyika kwa miezi miwili au zaidi kabla ya kuanza mavuno hali iliyopelekea ugumu wa kufanya malipo ya kodi hasa ikizingatiwa wananchi wanakodi ni hao hao.
4. Mwitikio mdogo wa wasimamizi wa mashamba ya eka wakati wa mnada na baadae kulalamika kwamba mashamba wanayoyasimamia yanakodishwa bila wao kupewa fursa ya kuyakodi.
5. Kuchanganywa mashamba zaidi ya moja na kumilikiwa na mtu mmoja kwa mwamvuli wa eka tatu.
6. Kuna mikataba ambayo imeonekana ina saini ya Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi kwa kipindi ambacho alikuwa amesha ondoka madarakani.
7. Waliokodi mashamba wengi wanalalamika kwamba mashamba yao yamechumwa na wasimamizi wa mashamba. Hali hii inatokana na mazoea ya muda mrefu ya mtu kuchuma au kukodisha shamba lake.
8. Wananchi wazalendo waliojitolea kusaidia uibuaji wa mashamba wanalalamikia kutopewa asante.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kufanya malipo ya kifutajasho mapema kwa wananchi wanaostahiki ili kuhamasisha wananchi kuyatunza vyema mashamba hayo.
2. Kamati inaishauri Serikali kuendelea na jitihada za kuwaelimisha wananchi juu ya umiliki wa mashamba ya eka tatu.
3. Kamati inaishauri Serikali kuweka mpango maalumu wa kuyapima na kuyagawa upya mashamba ya eka tatu.
4. Kamati inaishauri Wizara kwamba misimu ya karafuu inayokuja ni vyema mashamba yote yakakodishwa kwa mnada ili kuwa na ushindani mkubwa zaidi na hatimae kuongeza mapato ya Serikali.
5. Kamati inaishauri Serikali ifanye mapitio ya mikataba iliyotolewa ili kuwaondoshea usumbufu wananchi.
6. Kamati inaiomba Serikali iteue kamati ya Watendaji au Taasisi maalum itakayoweka utaratibu madhubuti wa ukodishaji wa mashamba ya Serikali ya eka tatu.
7. Kamati inaishauri Wizara kuwekwe utaratibu maalumu wa uwekaji kumbukumbu za shehia ili kuwawezesha masheha wanaostahafu kukabidhi taarifa za shehia kwa ukamilifu.

4.5 MSITU WA HIFADHI YA TAIFA WA KIWENGWA

Kamati inaipongeza Wizara na Serikali kwa jumla kwa maamuzi yake ya busara ya kuupandisha hadhi Msitu wa Kiwengwa kuwa ni miongoni mwa hifadhi tano kubwa kwa upande wa kisiwa cha Unguja zinazoendeshwa kwa mashirikiano ya Serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka na vikundi kumi vinavyoizunguka hifadhi hiyo ambavyo ni Pongwe, Kiwengwa, Bambi, Pangeni, Pwani Mchangani, Kandwi, Upenja, Kilombero, Tunduni na Mchangani.

Msitu huo una ukubwa wa hekta 3,406 ambao umepandishwa hadhi na kutangazwa rasmi kuwa hifadhi ya Taifa mwaka 2002. Hifadhi hiyo ya Taifa ina umuhimu wa kipee kwani imekusanya viumbe adimu vikiwemo miti, wanyama na ndege kadhaa. Kutokana na kuwepo kwa hifadhi ya msitu wa Kiwengwa, itaiwezesha Serikali kulinda, kusimamia na kuhifadhi ipasavyo maliasili na kutunza vyanzo vya maji vilivyomo pamoja na kuendeleza utalii wa kimaumbile kupitia vivutio mbali mbali vikiwemo mapango, wanyama, mila na utamaduni wa wenyeji wa maeneo hayo. Aidha, Serikali kupitia utalii wa kimaumbile, itaweza kupata fedha za kigeni na kuongeza mapato yake kufuatia michango au ada zinazotozwa na wageni wanaoutembelea msitu huo. Kwasasa watalii wapatao 90 hadi 150 huwa wanautembelea msitu huo kwa kila mwezi. Pamoja na umuhimu uliopo katika msitu huo lakini bado kuna changamoto zifuatazo zinazoikabili Idara inayosimamia msitu huo.

CHANGAMOTO

1. Kuvamiwa kwa Msitu huo na baadhi ya wananchi wanaotoka nje ya maeneo hayo kwa kufanya shughuli za ufugaji, ukulima na kuanzisha makaazi kinyume na utaratibu uliowekwa.
2. Upungufu mkubwa wa wafanyakazi walioajiriwa kuiendesha na Hifadhi hiyo

huhusan walinzi ambapo kwasasa wanao walinzi 14 tu.

3. Upungufu wa vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri hususan kwa askari wanaofanya doria katika msitu huo.
4. Kutopata mashirikiano mazuri na baadhi ya vyombo vya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yanayowakabili kwani wanazo kesi nyingi zilizopo Mahakamani lakini bado hazijatolewa hukumu.
5. Kupotea kwa baadhi ya wanyama wakiwemo Paa nunga ambao kwa utafiti walioufanywa wamebakia 300 kutoka 3,000 waliokuwa nao.
6. Upatikanaji mdogo wa fedha za kuendeshea Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka.
7. Kuendelea kuwepo kwa matumizi mabaya ya misumeno wa moto pamoja na uvunaji haramu wa Maliasili zisizorejesheka.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ihakikishe inaajiri watendaji wa kutosha wakiwemo walinzi ili kuhakikisha msitu wa Kiwengwa unapatiwa ulinzi wa kutosha,.
2. Wizara ihakikishe inajenga hoteli ya vyakula vya Kizanzibari na vyenginevyo ili watalii wanaofika katika msitu huo waweze kujipatia chakula.
3. Wizara ijenge 'zoo' ndogo ya wanyama katika msitu huo ili watalii wanaofika katika msitu huo waweze kujionea wanyama mbalimbali wanaopatikana Zanzibar.
4. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango wakae pamoja kuangalia uwezekano wa kuibakisha asilimia thalathini (30%) ya michango inayotokana na Mfuko wa Uendelezaji Misitu katika Idara ya Misitu na Maliasili zasizorejeshekakwa ajili ya uimarishaji na uendelezaji wa shughuli za Msitu huo.
5. Wizara kupitia Idara yake itoe elimu kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yaliuzunguka msitu juu ya upandaji miti katika maeneo yao na kwa matumizi yaon ili kuepusha uvamizi wa msitu wa hifadhi ya Kiwengwa,
6. Wafanyakazi wapatiwe vyombo vya usafiri ambavyo vitawasaidia kutekeleza majukumu yao kwani kwasasa wana gari moja ya Mkurugenzi lakini hawana gari kwa ajili ya kazi za uhifadhi wa Msitu huo. Kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na vikosi vya ulinzi na usalama nchini, Wizara isimamie vyema taratibu za ukamataji na uangamizaji wa misumeno ya moto nchini, ili kuiepusha nchi yetu kuwa jangwa.

4.6 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Kamati inaipongeza Wizara kwa jitihada inazozichukua za kuhakikisha wanaajiri wafanyakazi wa kutosha watakaofanyakazi za kawaida na kitaalamu ndani ya Wizara hiyo. Kwa bahati mbaya, Wizara imewasilisha maombi mengi ya kuajiri wafanyakazi katika Wizara inayohusiana na Utumishi wa Umma pasi na kuwepo mafanikio. Kila mwaka Wizara inafanya maombi ya mahitaji yao ambapo ajira ya mwisho wamepatiwa mwezi Septemba mwaka 2017 ambapo waliajiri wafanyakazi 48 (Unguja 35 na Pemba 13) kwa maombi ya nafasi za kazi ya mwaka 2015. Hivyo, kuna mahitaji makubwa ya wafanyakazi katika Wizara hiyo hasa ukizingatia wafanyakazi wengi wameshastaafu au

wanakaribia kustaafu.

Moja kati ya Wizara iliyo na wafanyakazi wengi na wenye viwango vikubwa vya elimu ni Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi lakini bado kuna mahitaji makubwa ya wafanyakazi hususan katika fani za kitaalamu katika sekta ya madaktari wa mifugo

CHANGAMOTO

1. Bado Wizara haijayatambua mashamba yote yanayomilikiwa na Wananchi kinyume na utaratibu.
2. Bado Wizara inakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi katika Taasisi na Idara zake suala ambalo linakwaza ufanisi wa Taasisi na Wizara kwa ujumla.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ifuatilie kwa karibu maombi ya nafasi tupu ambazo tayari imeshaziomba Wizara inayoshughulikia Utumishi wa Umma.
2. Kamati inaendelea kuielekeza Wizara kwamba pamoja na mashamba kadhaa ambayo imeweza kuyambulia lakini bado yapo mashamba mengine hayajatambuliwa. Hivyo, Wizara iongeze kasi ya kuyatafuta mashamba hayo hususan kwa kushirikiana na Masheha waliomaliza utumishi wao.
3. Wizara inashauriwa kuwa makini na Taasisi za kibenki zitakazokubaliwa kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa Wakulima kwani wakulima wetu ni masikini sana.
4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuzisambaza Ripoti za Hali ya Chakula Zanzibar kwa Mwaka 2016 hadi 2017 kwa Wadau mbali mbali wakiwemo Wajumbe Bazara la Wawakilishi na wananchi ili umma uelewe muelekeo mzima wa upatikanaji na ukosekanaji wa chakula katika nchi yetu.

4.7 MAENDELEO YA UVUVI

4.7.1 UZALISHAJI WA ZAO LA MWANI

Zanzibar ni kisiwa ambapo wananchi wake pamoja na mambo mengine wanalima mwani kwa ajili ya kujikimu katika maisha yao. Maeneo mbalimbali yakiwemo ya Chwaka, Bwejuu na Nungwi yanatumika sana kulima zao hilo. Pamoja na juhudi zinazofanyika za kuzalisha mwani lakini bado wakulima wake wanasumbuliwa na tatizo la kuwepo kwa bei ndogo ya zao hilo ukilinganisha na nguvu inayotumika katika uzalishaji wake.

Licha ya changamoto hiyo, Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa juhudi ambazo inaziendeleza za kuhakikisha kilimo cha mwani kinakuwa rasilimali kubwa ya kuimarisha kipato cha wananchi na uchumi wa nchi yetu. Kwani Wizara tayari imeshaiona changamoto hiyo na imeshatafuta Mtaalamu kutoka Indonesia wa kufanya utafiti ili waweze kutambua sababu inayopelekea zao hilo kukumbwa na maradhi na kutafuta dawa ya kutibu na kuondosha kabisa tatizo hilo ili wakulima wetu waweze kuzalisha mwani mwingi na ulio bora.

CHANGAMOTO

1. Bado uzalishaji wa zao la mwani Zanzibar unalimwa kienyeji.
2. Kuwepo kwa wadudu wanaorudisha nyuma uzalishaji wa zao hilo.
3. Kuwepo kwa bei ndogo ya ununuzi wa mwani Zanzibar.
4. Kuwepo kwa uvuvi haramu katika maeneo tofauti ya Zanzibar.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ihakikishe kwamba baada ya Mtaalamu huyo kumaliza utafiti wake, majibu wapatiwe Wananchi ili waweze kutambua tatizo linaloikumba zao hilo na njia ya kutatua tatizo lao.
2. Wizara ichukue juhudi kuhakikisha Wakulima wa Mwani wanalima kitaalamu kwa lengo la kujiongezea kipato chao.
3. Wizara iwafundishe wakulima wa Mwani njia mbadala za kuutumia mwani kuzalisha bidhaa nyengine bora zikiwemo sabuni na vyakula mbalimbali.
4. Wizara ihamasishe ulimaji wa mwani wenye soko kubwa ulimwenguni pamoja na kuwapatia wakulima wa Mwani vitendea kazi.
5. Wizara ifanye juhudu za makusudi kuliimarisha zao la mwani kwa kushajihisha ulimwaji wa mwani wa kisasa wenye bei na soko kubwa duniani ambao unalimwa katika maji mengi.
6. Wizara ihakikishe inawapatia mikopo Wajasiriamali wa vikundi vya Mwani ili waweze kuendeleza ukulima wa kisasa wa zao hilo.
7. Wizara iwapatie wakulima wa mwani mbegu mpya za kilimo hicho ili waweze kulima kisasa.

4.7.2 SHUGHULI ZA UANIKAJI DAGAA

Kamati ilitembelea katika maeneo mbali mbali yakiwemo Maruhubi, Ndagoni na Mangapwani kujionea shughuli za uanikaji wa dagaa zinazoendelea katika maeneo hayo. Aidha, Kamati iliarifiwa kuwa Wizara inajiandaa kununua mashine za kukaushia dagaa ili kuifanya shughuli hiyo kuwa ni rahisi zaidi. Katika juhudi za kuwapatia masoko wanaifanya biashara hiyo, Wizara imewafunza wajasiriamali kadhaa juu ya namna bora ya kuanika vizuri kwa kutumia chanja maalum ili wauze gadaa hilo kwa bei nzuri sokoni. Zifuatazo ni miongoni mwa changamoto ambazo biashara hiyo inakabiliana nazo:-

CHANGAMOTO

1. Pamoja na utaalamu waliopatiwa baadhi ya waanika dagaa, uanikaji wa dagaa kwa njia ya chanja unahitaji mtaji mkubwa na hivyo wafanya biashara wengi hushindwa kuzimudu gharama zake.
2. Eneo liliopo karibu na shughuli hizo za dagaa hapo Maruhubi linakabiliwa na tatizo sugu la umwagaji wa kinyesi na kulifanya eneo hilo kuwa hatarishi kwa afya ya wafanya biashara na walaji wa dagaa.
3. Bado wafanyabiashara hao wanatumia njia za kizamani za kuanika dagaa chini na kushindilia kwa miguu.
4. Waanika dagaa wa Ndagoni wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa mikopo nafuu itakayowawezesha kununua mashine ya kisasa ya ya kukaushia dagaa hususan katika kipindi cha mvua kubwa.

5. Ukosefu wa vifungashio bora vya dagaa hupelekea kuharibika dagaa hilo muda mfupi baada ya kuingia sokoni.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ihakikishe inanunua mashine za ukaushaji wa dagaa na kuzitumia kwa kuwapatia huduma waanikaji na wananchi kwa ujumla.
2. Wizara kupitia Serikali ya Wilaya ya Mjini wasimamie ipasavyo diko la maruhubi na kuweka taratibu maalum ili kulinusuru diko hilo na uvamizi wa watu wabaya kutoka sehemu mbali mbali.
3. Kamati inasisitiza umuhimu wa kufuata kanuni za afya kwa kuacha kabisa kumwaga kinyesi katika eneo la Maruhubi na badala yake kumwaga kwenye eneo lililotengwa kwa kazi hiyo huko Kibele.
4. Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ifanye utafiti juu ya biashara ya dagaa katika nyanja zake zote ikiwemo uvuaji, uanikaji, uhifadhi na ufungaji pamoja na masuala ya masoko ya ndani na nje ya nchi.
5. Wizara ihakikishe inadhibiti bei inayotolewa ovyo na waanika dagaa huko Mangapwani.
6. Wizara ilifuatilie na kulipatia ufumbuzi suala la kuondoshwa kwa waanika madagaa huko Mangapwani kwa maslahi ya Serikali na Waanikaji hao.

4.8 MAENDELEO YA KILIMO

Wizara ya kilimo inajukumu kubwa la kuhakikisha kilimo kunaimarishwa kwa kuendeleza tafiti za kilimo, kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za kilimo kwa wakulima, Kuhakikisha upatikanaji wa chakula na lishe ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Kamati inaendelea kuthamini juhudi za Wizara ya kilimo na kuisisitiza katika mambo yafuatayo:

4.8.1 UENDELEZWAJI WA SHAMBA LA RAZABA

Katika mpango mpya wa kuliendeleza shamba la RAZABA ambao Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Tanzania Bara (NHC) imeamua kulipima eneo hilo kwa ajili ya kuandaa mpango mpya wa matumizi ya ardhi kulingana mpango wa Mji wa Bagamoyo.

CHANGAMOTO

Kukwama kwa 'Memorandum of Understanding' (MoU) katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ifuatilie 'Memorandum of Understanding' (MoU) iliyopo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili Wizara iweze kuendelea na hatua za utekelezaji.
2. Wizara ichukue juhudi za makusudi kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kufika na kujionea uwepo wa shamba hilo na ukubwa wake ili kamati iweze kuishauri Serikali ipasavyo.
3. Mara baada ya kumaliza kupimwa kwa shamba hilo, Wizara ihakikishe utekelezaji wa 'Master Plan' mpya ya eneo hilo.

4.8.2 KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO - MATANGATUANI

Kituo kinawafanyakazi 32 wakiwemo wataalamu 17 na wengine ni "supporting staff". Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2017, kituo kimejenga ukumbi wa mikutano, wamefanya tafiti mbili; moja ya ukulima wa Muhogo kwa kuangalia kwanini baadhi ya Wakulima hao wanafanikiwa na wengine hawafanikiwi na tafiti nyengine inahusu miche ya Mikarafuu ambayo imetolewa miaka 10 iliyopita bado wakulima wanaiendeleza (ipo hai) au haipo.

Ili kilimo chetu kiweze kupiga hatua, Seriakali lazima ijikite zaidi na masuala ya utafiti kwani kilimo chetu siku hizi kinakabiliwa na changamoto za kuvamiwa na wadudu waharibifu wanaorudisha nyuma juhudi za wakulima wetu; mfano mzuri ni kilimo chetu cha mwani. Hivyo, Wizara lazima iandae maabara ya kisasa, yenye vyombo makhsus, wataalamu pamoja na kuweka mazingira bora kwa wafanyakazi na vifaa husika. Mbali na mambo yote ya msingi yanayohitajika kuwepo katika kituo cha utafiti bado kituo cha Matangatuani kinachangamoto zifuatazo:-

CHANGAMOTO

1. Ukosefu wa usafiri kwani Ofisi ina gari moja kongwe takriban ya miaka 10 iliyopita.
2. Ukosefu wa Ofisi ya kufanyia kazi kwani huwa wanatumia Ofisi ya Maabara.
3. Ukosefu wa vifaa vinavyotumika maabara.
4. Bado kituo kwasasa kimefanya tafiti tangulizi (baseline survey) na baada ya matokeo ya tafiti hizo ndio watafanya tafiti za kimaabara.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inataka Wizara iipatie vifaa vya Maabara kituo cha Matangatuani ili kutoa matokeo ya utafiti ya kitaalamu.
2. Kituo kifanye mawasiliano na FAO kwani wanaweza wakawasaidia kwa kuwapatia vifaa vya utafiti wanavyovihitaji.
3. Uzio wa Maabara ufanyiwe matengenezo ili Maabara hiyo ipate hifadhi iliyo nzuri.
4. Wizara ihakikishe inatengeneza jengo kwa ajili ya Ofisi ya kituo ili wafanyakazi waweze kufanyakazi zao katika mazingira mazuri.
5. Wizara ihakikishe inatangaza taarifa za matokeo ya utafiti wa mbegu za Muhogo na Mikarafuu ili ziweze kuwafikia wakulima wajue mbegu gani zinafaa kutumika na zipi hazifai.

4.9 KILIMO CHA MPUNGA WA UMWAGILIAJI MAJI

Katika juhudi za kufikia lengo la kujitosheleza kwa chakula, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji katika sehemu mbali mbali nchini. Ni ukweli uliowazi kwamba wakulima wameshajihika sana na kilimo cha umwagiliaji maji kwani ukilinganisha na kilimo cha kutegemea mvua, wakulima huwa wanatumia nguvu nyingi na uzalishaji huwa mdogo sana. Vile vile, kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji wakulima huweza kulima mara mbili au zaidi kwa mwaka mmoja. Katika kutathmini na

kusimamia Kilimo cha umwagiliaji maji, Kamati ilifanikiwa kutembelea mabonde kadhaa yakiwemo:

4.9.1 BONDE LA CHEJU

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilibahatika kulitembelea bonde la Cheju kujionea harakati za shughuli za kilimo zilizokuwa zikifanyika katika bonde hilo. Kamati iligundua kwamba wakulima wa bonde hilo wamegawika ambapo wapo wanaolima ukulima shadidi na wengine bado wanaendelea na kilimo cha kutegemea mvua za msimu. Aidha, changamoto kadhaa zilikuwa zinawakabili wakulima wa eneo hilo zikiwemo zifuatazo:

CHANGAMOTO

1. Bado kuna wakulima hawajahamasika na ukulima wa kilimo shadidi na wanaendelea na kilimo cha zamani pamoja na kuelezwa faida kubwa iliyopo
2. Wakulima wanaendesha shughuli zao kwa kutumia zana za asili ambazo hutumia nguvu nyingi na kuchukua muda mrefu jambo ambalo linakwamisha shughuli nyengine za kimaendeleo.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) itafute njia mbadala ya uwekaji wa nguzo za umeme katika eneo hilo kwani imebainika kuwa maumbile ya ardhi ya bonde la Cheju husababisha nguzo kuinama siku chache baada ya kuwekwa na hivyo kuigharimu Serikali na kuhatarisha maisha ya wakulima na wananchi kwa ujumla.
2. Wizara ichukuwe juhudi za makusudi kuwapatia wakulima wa mpunga wa bonde la Cheju vifaa vya kisasa ili kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa.
3. Wizara ihakikishe inapeleka mashine ya kuweka sawa maeneo ya kilimo cha mpunga “Levilling meshine” ili kuwezesha maji kubakia na kuenea bonde lote pamoja na trekta kulima kwa urahisi zaidi.
4. Kamati inaiagiza Wizara kuwaunga mkono wakulima wa Cheju kwa kuwajengea kwa saruji mtaro wao wa umwagiliaji maji ambao tayari wameuchimba kwa njia ya kujitolea.
5. Wizara iwaelimishe Wakulima kuhusu kulima kilimo cha biashara na kuachana na kilimo cha kujikimu.

4.9.2 BONDE LA MANGWENA

Bonde la Mangwena lina hekta 9.8 ambalo limeanza kutumika mwaka 1986, bonde hilo linatumika kwa kulima mpunga wa umwagiliaji maji na sehemu nyengine wanalima kwa kutegemea mvua za msimu. Sehemu ya umwagiliaji maji, miundombinu yake imetengenezwa kwa mchango wa Serikali ya Japan kwa mashirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali ya Japan ilijenga mitaro mita 600 na ikachimba kisima wakati SMZ ilileta umeme, ikatoa nguvu kazi, ikawachukua Wakulima 18 kuwapeleka Moshi kupata mafunzo ya mbinu za ukulima bora na ikajenga barabara. Aidha, Tzs. 112 milioni za Japan na Tzs. 113 milioni za SMZ zilitumika kuyaimarisha mashamba hayo.

CHANGAMOTO

1. Kuingia kwa mchanga au kifusi katika bonde kunakotokana na kusukumwa na maji ya mvua yanayotoka juu milimani. Hali hio imetokea hivi karibuni baada ya kutengenezwa kwa Barabara iliyopita katika eneo hilo.
2. Kutotumika kwa mbolea ambayo imehifadhiwa pasi na kutumiwa na wakulima.
3. Wakulima wa bonde hilo huwa wanashindwa kujitokeza wakati wa kupatiwa mafunzo.
4. Banda wanalotumia wakulima kuhifadhia vitu vyao limefanya ufa kutokana na kukatika kwa barabara iliyosababishwa na maji ya mvua kurundikana.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara na Maofisa Wakuu wa kilimo watoe elimu kwa wakulima wa Bonde la Mangwena kuhusu umuhimu wa kutumia mbolea kwa wakati na kuacha kuziweka ndani.
2. Wizara ichukue juhudi kuhakikisha eneo la bonde la Mangwena lililobakia linajengwa miundombinu ili wakulima wote walime kilimo cha umwagiliaji maji.
3. Wizara inayoshughulikia Kilimo ikutane na Wizara ya Miundombinu kurekebisha eneo lililoharibika la Bonde la Mangwena ili kifusi kisiingie katika misingi ya umwagiliaji maji hususan katika kipindi cha mvua inaponyesha.

4.9.3 BONDE LA MPUNGA LA UKELE

Bonde la Ukele linapatikana karibu na bahari katika Wilaya ya Micheweni ambalo lilibahatika kutembelewa na Mheshimiwa Rais DK. Ali Mohamed Shein mnamo mwaka 2011 na kujionea athari ya maji ya bahari kwa mpunga unaolimwa bondeni hapo. Kufuatia ziara hiyo, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliagiza kujengwe tuta litakalozuia maji ya bahari kuingia katika bonde hilo na kuathiri mpunga. Mwezi Machi 2012, ujenzi wa tuta hilo ulikamilika na kuwafanya wakulima kurudi tena kwenye bonde hilo kwa ajili ya shughuli zao za kilimo cha mpunga ambazo zilikwama kwa takriban miaka kumi. Kamati inaunga mkono suala la bonde hilo kuingizwa kwenye mpango wa umwagiliaji maji ili kufanya matumizi sahihi ya maji ya mvua ambayo kwa sasa ni changamoto bondeni hapo.

CHANGAMOTO

1. Wizara ihakikishe tuta la kuzuia maji yasiingie katika bonde la mpunga linalindwa na kuhifadhiwa ili shughuli za kilimo nazo ziweze kuendelea kwani imeonekana uharibifu wa tuta hilo umetokana na kutowajibika ipasavyo kwa Kamati ya bonde hilo jambo ambalo linapelekea utunzaji usioridhisha wa tuta la kuzuia maji ya bahari ambalo limejengwa kwa gharama kubwa.
2. Kufuatia mvua zilizonyesha msimu huu, sehemu ya tuta hilo imeharibika na inahitaji matengenezo ya haraka ili kuwafanya wakulima wa bonde hilo kuendelea na kilimo cha mpunga kwa msimu huu.
3. Athari za mabadiliko ya tabia nchi ambazo zinapelekea maji ya bahari kuingia kwenye maeneo ya bonde hilo.
4. Ukataji wa mikoko unaofanywa na wananchi.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kufanya matengenezo ya haraka katika tuta la bonde hilo ili kuwapa fursa wakulima kuwahi kulima katika msimu wa masika na kujihakikishia kupata chakula cha kutosha.
2. Kamati inaishauri Kamati ya bonde hilo kuthamini juhudi za Serikali na kuziunga mkono kwa kulitunza kikamilifu tuta lililojengwa bondeni hapo ikiwa ni pamoja na kuteua watu maalum kwa ajili ya kufunga na kufungua mlango wa maji ya bahari.
3. Waziri wa Kilimo akae na Waziri wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Serikali ya Mkoa, Wilaya, Masheha na wadau wengine ili kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa bonde hilo.
4. Wizara ihakikishe inatoa uelewa kwa wananchi wa maeneo hayo kuhusu kuacha kukata mikoko na badala yake kuienzi iliyopo na kupanda mipya.

4.10 SHAMBA LA MIKARAFUU MAKUWE

Shamba la Makuwe ni shamba la Serikali ambalo lina hekta 79.9 sawa na plot 10, Shamba hilo ni la Mikarafuu na baadhi ya mazao mengine likiwemo minazi, limegawiwa katika sehemu kumi ili kurahisisha uimarishaji wake. Aidha, shamba hilo pia linaweza kupandwa pilipili, vanilla na minazi.

Shamba linahudumiwa na wafanyakazi sita lakini wanahitajika wafanyakazi 30 ili kuliendeleza ipasavyo na kupata faida iliyokusudiwa. Hadi Kamati inalitembelea shamba hilo limekodishwa kwa Tzs. 294 kwa njia ya tenda. Kikawaida, nazi zinapovunwa zinatumika kwa kuatikia miche ambapo mwakani wanapanga kuacha plot moja ya mikarafuu kwa ajili kuatika mbengu. Aidha, Balozi wa China ametoa 'offer' kwa Wizara inayoshughulikia Kilimo kuliimarisha zao la Muhogo kwani wanahitaji kiwango kikubwa cha bidhaa hiyo nchini kwao. Wizara kwa upande wake imefanya mawasiliano ili kujua ni aina gani ya muhogo ambao unahitajika kwa ajili ya soko hilo lakini bado Wizara haijajibiwa.

CHANGAMOTO

1. Wizara inakabiliwa na tatizo la wizi wa mazao ambapo hadi kamati inalitembelea shamba hilo kulikuwa na kesi mbili za wizi wa nazi zinaendelea.
2. Ukosefu wa maji katika shamba hilo.
3. Kuzeeka kwa mikarafuu mingi iliyomo shambani humo ni jambo linalohitaji kufikiriwa kwa kina na kupatiwa suluhisho la haraka kwani mikarafuu mipevu hupunguza mazao na mengine hufa.
4. Mwamko mdogo wa baadhi ya wakulima juu ya njia bora za ukulima wa mikarafuu.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kufanya juhudi maalum za kupanda wa mikarafuu mipya ili kuhakikisha mavuno makubwa zaidi yanapatikana katika siku zijazo.
2. Wizara ihakikishe upatikanaji wa maji katika shamba hilo unakua ni wa uhakika ili kuwafanya watendaji wake waweze kutekeleza shughuli zao ipasavyo.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuyazingatia mapendekezo ya uendelezaji wa shamba hilo lenye ploti kumi kwa kulipatia bajeti ya miaka mitatu ili kukabiliana na gugu linaloota kwa kasi kabla hata ya kumaliza kupaliliwa.
4. Wizara iwaelimishe watendaji wake na jamii kwa ujumla juu ya umuhimu wa kuitenganisha mikarafuu na mazao mengine ya chakula kama muhogo kwani Kamati imebaini kuwa ukulima wa muhogo ndani ya mashamba ya mikarafuu husababisha mikarafuu kufa.
5. Wizara iwatumie vijana wa JKU kwa kusafisha mashamba hayo ili kukabiliana na uhaba wa watendaji hadi pale watakapopatikana.
6. "Strategic Plan" ya Mashamba ya Makuwe ikamilishwe ili hatua za kuyaimarisha mashamba ziweze kufanyika.
7. Jengo la Ofisi ya Makuwe lifanyiwe matengenezo.
8. Tatizo la maji na wafanyakazi litatuliwe ili manung'uniko na maswali yaondoke.

4.11 WAKALA WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO

Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo umeanzishwa chini ya Hati ya Kisheria Namba 2 ya mwaka 2011 kwa ajili ya kusimamia na kuimarisha shughuli za karakana za Matrekta ziliopo Mbweni na Machomane Pemba ambapo kwasasa Wakala huo una jumla ya Matrekta 35. Aidha, Wakala imepokea Matrekta 10 mapya kutoka ubalozi wa Libya lakini yameshindwa kufanya kazi mara tu baada ya kufika kutokana na kutolewa baadhi ya vifaa huko yalipohifadhiwa. Wakala imepanga kununua vifaa hivyo na kuyatengeneza matrekta hayo ili yaweze kutoa huduma Unguja na Pemba ambapo hadi Kamati inapokea ripoti ya utekelezaji wa malengo ya bajeti, matrekta matatu yalikuwa yameshatengenezwa na yanafanya kazi. Mbali na mambo mengi ambayo Wakala imeyafanya lakini inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

CHANGAMOTO

1. Wakala umeanzishwa na Serikali lakini unafanya shughuli zake katika ardhi ya kukodi jambo ambalo linaifanya Wakala kutumia gharama kubwa kulipia kodi.
2. Kuchelewa kwa vifaa vya kufanyia matengenezo 'spare parts' kwa ajili ya matengenezo ya matrekta kunakwamisha huduma kwa wakulima.
3. Mashine za kuendeshea shughuli kuu za Wakala ni chakavu mno na zinakwamisha shughuli za matengenezo ya matrekta.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iipatie fungu lake la matumizi (vote) kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake kama zilivyoelezwa kwenye legal notice ya uanzishwaji wa Wakala huo.
2. Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia maombi ya hati miliki ya eneo hilo (title deed) ambayo tayari imewasilishwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.
3. Wizara ifuatilie suala la muundo wa Wakala "organization structure" ambayo hadi sasa bado haijapitishwa Serikalini.

4. Wizara itoe mafunzo kwa watendaji wa Wakala ili waache kufanya kazi kwa kutumia teknolojia ya zamani kwani imebainika kuwa shughuli za kiufundi zinazoendeshwa na Wakala huo zinafanywa kwa njia za kiasili zaidi.
5. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais la kuupatia Wakala jumla ya Matrekta 20 kutoka kampuni ya Mahindra ili kuzidi kuongeza nguvu katika utendaji wa Wakala hiyo na kuinua hali za wakulima wetu.
6. Kamati inaitaka Wizara kuhakikisha kuwa kitengo cha uchongaji wa mashine (mashine workshop) kinapatiwa zana kwa wakati na za kutosha ili kuondosha tatizo la upungufu mkubwa wa zana kiasi cha kutishia utendaji wa kitengo hicho.
7. Kamati inasisitiza kushirikishwa kwa mafundi husika kila wanapotaka kuagiza vifaa ili kupata vifaa bora na stahiki kwa maendeleo ya nchi yetu.
8. Wizara ihakikishe wafanyakazi wa Wakala wanatekeleza majukumu yao ipasavyo na wanazidisha mashirikiano miongoni mwao ili waweze kutimiza malengo waliyojipangia.

4.12 UATIKAJI WA MICHE

4.12.1 KITALU CHA MWERA

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haina budi kuipongeza Wizara ya Kilimo, Malisili, Mifugo na Uvuvi kwa kuliona hilo na tayari imeonesha nia na njia kwa wakulima wetu kwa kuandaa vitalu vyake na kutoa elimu kwa wananchi wengine kuendeleza shughuli ya uatikaji na uendelezaji wa miche ya miti mbalimbali ikiwemo Mikarafuu na Minazi.

Kamati yangu ilipata fursa ya kukitembelea Kitalu cha Mwera kinachoatika miche ya Mikarafuu na Matunda ambacho kinaendeshwa na kusimamiwa na Wizara inayoshughulikia Kilimo. Utaratibu unaotumika katika ugawaji wa miche hiyo ni kwamba kwa miche ya Mikarafuu inayozalishwa katika Kitalu hicho husambazawa katika Ofisi za Wilaya na kugaiwa kwa wakulima bila ya malipo yoyote. Aidha, kwa miche ya Matunda, Wizara huiuza kwa Wakulima wanaohitaji kwa gharama nafuu.

CHANGAMOTO

1. Ubovu wa nyavu wanazozitumia kuhifadhia mbegu dhidi ya jua kali.
2. Hawana maji ya uhakika kwani wanategemea maji ya Zawa na kisima cha mtu binafsi.
3. Hawana Ofisi inayoeleweka kwani jengo wanalolitumia kwasasa ni dogo, la udongo na limeezekwa makuti.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ihakikishe Kitalu hicho kinapatiwa maji ya uhakika kwa kuchimba kisima kitakachotumika kwa kumwagilia maji mbegu au miche iliyoatikwa.
2. Wizara itafute fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya kisasa ili kuondosha tatizo la kuwa na Ofisi ya kudumu.
3. Wizara ihakikishe inawapatia nyavu za kuatikia miche katika Kitalu hicho kupitia fedha wanazoingiziwa.

4. Kamati imeshauri eneo la uzalishaji miche liliopo Mwera lizungushiwe uzio kuzuia uvamizi wa Wanyama na Watu wasiohusika kuingia katika eneo hilo.

4.12.2 KITALU CHA CHANJAANI MWANATOJO

Hiki ni miongoni mwa vitalu vikubwa vilivyopo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba ambacho kina jumla ya miche 28,575 ya mikarafuu ambayo imezalishwa kwa nguvukazi ya watendaji wanane. Kiwango cha ustawi wa miche hiyo ni asilimia 53 baada ya kutoka kitaluni ambayo kiuhalisia huwa inapanda au kushuka kulingana na huduma zitakazotolewa na mkulima mwenyewe.

CHANGAMOTO

1. Sera ya Serikali ya utoaji wa bure miche ya mikarafuu iliwekwa kwa nia njema kabisa lakini inatumiwa vibaya na baadhi ya wanajamii kwani huchukuwa miche vitaluni na kuitelekeza mashambani.
2. Uchache wa elimu juu ya upandaji na ushughulikiaji wa mikarafuu katika hatua mbalimbali unasababisha upungufu wa mavuno ya karafuu.
3. Kamati imebaini kuwa mikarafuu mingi iliyopo nchini ni mikongwe mno na hivyo kupunguza kasi ya kuzaa na myengine imeanza kufa.
4. Watendaji wa kituo hicho wanakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi kama viatu vya 'rain boots' na maji ya kumwagilia katika msimu wa Kiangazi. Pia, ukataji wa miti ovyo ndani ya eneo la kituo hicho unarudisha nyuma juhudi za wafanyakazi hao na Serikali kwa ujumla.
5. Kuwepo kwa madeni makubwa ya stahiki za likizo kwa watendaji wa kituo hicho ni jambo linalowasononesha watendaji hao.
6. Ukosefu wa huduma za vyoo katika kitalu hicho kunarudisha nyuma ufanisi wa wafanyakazi hao.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iendelee na juhudi zake za kuwaelimisha wanachi juu ya umuhimu wa kuitunza miche ya mikarafuu mara baada ya kukabidhiwa ili kutumia vyema rasilimali za nchi kwa maslahi ya Taifa.
2. Utafiti wa kina unahitajika ili tujuwe ni kwa kiasi gani hasa tunahitaji mikarafuu mipya ili tuweze kupata tija zaidi na kujiletea maendeleo.
3. Wizara ihakikishe inajenga vyoo vya kutosha na vya kisasa ili kuwaepusha wafanyakazi wetu na uwezekano wa kupata maambukizi mbalimbali.

4.13 WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI - PEMBA.

Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo - Pemba kwa juhudi ilizozifanya hususan za kutekeleza ushauri na maagizo ya Kamati kwa kujenga jengo la kituo cha Mifugo cha Chamanangwe pamoja na kuweka maji na umeme. Utengenezwaji wa banda hilo umewawezesha wakulima na wafanyakazi kutekeleza majukumu yao katika mazingira mazuri. Pamoja na juhudi hizo bado Ofisi ya Afisa Mdhamini inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

CHANGAMOTO

1. Wakulima kuendelea kulima kilimo cha zamani cha kutegemea mvua na kuacha kulima kilimo cha kisasa cha kibiashara na chenye tija kubwa.
2. Baadhi ya mashamba bado hayajatambuliwa na Wizara.
3. Upungufu wa wafanyakazi katika Idara na Taasisi nyingi zilizopo Pemba.
4. Kukosekana kwa hewa ya Nitrogen katika Maabara - Pemba.
5. Kuchelewa kuwasili kwa vifaa vya mwani.
6. Upungufu wa wafanyakazi katika sekta zake.
7. Mabadiliko ya hali ya hewa yamepelekea baadhi ya mabonde ya umwagiliaji maji kuchelewa kulimika.

MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ihakikishe inaajiri wafanyakazi wapya na kuwapeleka katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa wafanyakazi hao.
2. Ofisi ya Afisa Mdhamini ihakikishe Afisa Msimamizi wa kituo cha utafiti wa Mifugo cha Chamanangwe anapatiwa usafiri ukizingatia ni mwanamke.
3. Wizara iendelee kuchukua juhudi za kuyatafuta na kuyatambua mashamba ambayo bado yanamilikiwa na wananchi kinyume na utaratibu.
4. Ofisi ya Afisa Mdhamini ihakikishe tatizo la upatikanaji wa hewa ya Nitrogen katika maabara linatatuliwa.
5. Ofisi ya Afisa Mdhamini ihakikishe inaikamata misumeno ya moto ambayo inateketeza hata mikarafuu mibichi.
6. Afisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo na Afisa Mdhamini wa Wizara inayoshughulikia miundombinu wahakikishe wanaijenga barabara iliyopita katika bonde la Makombeni Pemba ambayo zimehabika kutokana na mvua.
7. Ofisi ya Afisa Mdhamini iwahimize wakulima kulima na mazao mengine ambayo yanaweza kuoteshwa katika mashamba ya Alizeti ikiwemo kunde, mtama, choroko na viazi vitamu.
8. Ofisi ya Afisa Mdhamini ihakikishe inawapatia wakulima maeneo zaidi ya kulima Alizeti.
9. Ofisi ya Afisa Mdhamini iwawezeshe wakulima kiutaalamu ili waweze kufuga nyuki katika maeneo yanayozalishwa Alizeti kwa vile nyuki huwa hawaadimiki katika maeneo hayo.
10. Wizara ifanya utafiti kugundua unapolima muhogo karibu na mikarafuu husababisha mikarafuu kufa. Hivyo kukifanyika utafiti tunaweza kujua umbali ambao unahitajika kuwepo baina ya mkarafuu na panapostahikli kupandwa muhogo.
11. Wizara imewasisitiza Kamati za Wilaya, Wananchi na Masheha ambao wamemaliza muda wao kutoa ushirikiano katika kuyatafuta na kuyatambua mashamba hayo kwa kutoa taarifa Wizarani.

SEHEMU YA TANO

5.1 HITIMISHO

Kwa ujumla, Kamati imefanikisha majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa kazi zake ilizojipangia katika Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo zilizoainishwa katika ripoti hii. Kamati inazipongeza Wizara na Taasisi hizo kwa mashirikiano yao ya dhati kwa Kamati katika kufanikisha kazi zake pamoja na juhudi zinazochukuliwa katika utekelezaji wa kazi zao.

Kamati pia inapenda kutoa shukurani kwa wale wote waliofanikisha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na pia kuwezesha taarifa za Kamati kutayarishwa na kuwasilisha kunakohusika. Kamati inawashukuru kwa dhati viongozi na watendaji wote wa Serikali na wa Baraza la Wawakilishi kwa utendaji bora wa shughuli zao za kila siku.

XXXXXXXXXXXXX *Mwisho* XXXXXXXXXXXXX